Kuwezesha Elimu

Chapisho la 10, Aprili 2006



Toleo Maalum: Elimu ya Ualimu

www.eenet.org.uk

EeNET
Enabling Education Network

Yaliyomo

Habari za Shirika la EENET 3
Uhariri – Msisitizo kwa Elimu ya Ualimu 5
Wazo linaloongelewa 8
Ndiyo, Nilifanya! Uzoefu wangu Binafsi katika Darasa-Jumuishi 10
Kuwashirikisha Watoto-wafanyakazi katika Elimu, Yemen 12
Kuunda upya Mfumo wa Elimu wa Kisovieti, Kyrgyzstan 14
Mafunzo ya Elimu-Jumuishi, Papua New Guinea 18
Mafunzo ya Ualimu, Uganda 20
Kubadilisha Namna Tunavyofundisha, Burkina Faso 22
Mtizamo wa Wanafunzi kuhusu Sifa za Mwalimu Bora, Uingereza 25
Kujitathmini na Ujumuisho, Bahamas 28
Kuyafanya Mazingira ya Kujifunzia Yavutie zaidi, Palestine 30
Kuchambua Vikwazo vya Elimu Vijijini, Chile 32
Mtandao wa Elimu-Jumuishi Nchini Gambia 37
Kuwapa Mafunzo Walimu Walemavu, Msumbiji 39
Kubadilisha Mfumo na Elimu Mashuleni: Kutumia ‘Vigezo vya Ujumuisho’ Nchini Afrika Kusini 41
Kufanya Kazi pamoja na Wazazi Nchini Uganda 43
Kuzingatia Sera: Iran 45
Habari za Kikanda 47
Masaili ya EENET 49
Barua/Barua-pepe zako 51
Machapisho Muhimu 53

Habari za Shirika la EENET

Siku moja katika maisha kwenye tovuti ya EENET: 2 Machi 2006

EENET inatumia mtandao mpya kuchanganua takwimu za tovuti yake. Yafuatayo ndiyo yaliyotokea siku hiyo kwenye tovuti yetu:

- Watu 356 walitumia tovuti siku hiyo
- Kutoka nchi mbalimbali 47, ishirini na tano zilikuwa nchi za kusini (53%), ambazo zilifanya 26% ya watumiaji wetu.
- Tano ya nchi kumi za mwanza katika watumiaji wa tovuti zilikuwa za kusini: Ufi lipino (ya 4), Brazili (ya 7), Mexico (ya 8), Afrika ya Kusini (ya 9), India (ya 10)
- Wageni 356 waliweza kusoma kurasa/matini mbalimbali 207
- Na moja iliyowavuta wengi ilikuwa 'Ndoa katika umri mdogo na Elimu' – makala iliyopo katika Chapisho Na.7.

EENET inazidi kuhamasisha uelewa zaidi kuhusu ndoa za mapema zinavyowanyima wasichana haki yao ya elimu. Tunakaribisha wasomaji wetu kuongeza makala nyingi zaidi kuhusu suala hili ili hatimae tovuti yetu iweze kukidhi haja ya wasomaji wetu.

Tovuti ya EENET inachangia kwa hakika kuhusu lengo letu la kubadilishana habari na nchi za kusini, japokuwa upatikanaji wa mtandao/intaneti sio sawa baina ya nchi za Kusini na zile za Kaskazini. Katika mwezi mmoja tu watu kutoka nchi 145 waliweza kutumia tovuti; 87 kati yake (60%) zilikuwa nchi za kusini.

Tovuti ya EENET kwenye CD-ROM

Kama hauna mtandao, kwa sasa tovuti yetu inapatikana pia kwenye CD-ROM. Teknolojia-jumuishi imetusaidia bila gharama yoyote kwa EENET na vilevile kuna kanda/diski zenye makala mbalimbali kutoka Kongresi la Elimu-jumuishi na Elimu-saidizi la mwaka 2005. kama unahitaji kupata nakale moja, tuwasiliane tafadhali.

Maandalizi ya Sherehe ya kila Mwaka

Mwaka 2007 EENET itakuwa imefikisha miaka 10, na tunawaalika wasomaji wetu wote kutusaidia kusherehekea! Teknolojia-jumuishi (Tovuti mfadhili wetu) itakuwa nayo inasherehekea hafla ya kumi na itakuwa ndiyo mwenyeji wa tukio hili la pamoja mnamo Januari 2007 ambapo wanatarajia kutoa ramani ya dunia inayoonesha wasomaji wa EENET wanakoishi. Tungependa kama utatutumia kadi, picha, au

mchoro (wako mwenyewe au uliochorwa na watoto) ukionesha unakoishi, unakofanya kazi, au unakosoma (Tarehe ya mwisho: 1 November 2006 na kumbuka kuandika jina lako/anwani nyuma ya picha au mchoro wako). Picha hizi zitaoneshwa kwenye ramani ya dunia. Kila atakayetutuma picha /mchoro atapata zawadi ya bure ya matini za Elimu-jumuishi, zilizofadhiliwa na Teknolojia-jumuishi. Na kama una mawazo ya ziada kuhusu kusherehekea mwaka wa 10 wa kuundwa kwa EENET ulimwenguni kote, tafadhali wasiliana nasi.

Wananyakazi wa EENET

Tangu mwezi Machi 2005, Susie Miles amekuwa ndiye Mkurugenzi wa Programu ya Shahada ya Uzalimili ya Elimu katika Elimu Maalum na Elimu-jumuishi katika Chuo Kikuu cha Manchester. Hata hivyo bado ana dhima ya ushauri katika EENET ingawa siyo mratibu wake tena. Ingrid Lewis ndiye Mratibu wa EENET kwa sasa ijapokuwa kaajiriwa kwa siku mbili tu za kila wiki. Uwezo wa utendaji kazi katika ofisi yetu umepungua kweli. Tunajitahidi kuendesha ofisi kwa kadiri tuwezavyo, lakini tungependa kuajiri mtumishi wa pili kama fedha zingepatikana.

Picha za Jarida na:
(kwa juu ya ukurasa) EENET (mzunguko wa saa kutoka juu kushoto): Boris Herger/Save the Children; Stuart Freedman/Network Photographers/Save the Children; EENET; Dan White/Save the Children; Danladi Mamman/GCEN
(picha ya katikati) EENET.

Shukurani
Shirika la EENET linayashukuru mashirika yafuatayo kwa kulisaidia kifedha katika uandaaji na utoaji wa Toleo hili:

- Norwegian Association of Disabled (Shirika la Kinorwei la Watu Wasiojiweza)
- Operation Day’s Work (Norway) (Shirika la Siku ya Operesheni ya Kazi Norway
- Save the Children UK (Shirika la Okoa Watoto, Uingereza)
- World Vision UK (Shirika la Taswira ya Dunia, Uingereza)

Uhariri – Msisitizo kwa Elimu ya Ualimu

Kwa Nini Mkazo uwe kwenye Elimu ya Ualimu?

Kila mwaka Kampeni ya Elimu Duniani (KED) huendesha juma zima la vitendo kuhamasisha juu ya suala mahsusi katika elimu. 'Kampeni ya Elimu Duniani (KED) ni muunganiko wa mashirika yasiyo ya serikali na vyama vya walimu kutoka zaidi ya nchi 150 ambazo huamini kuwa elimu bora inaweza kupatikana. Kampeni ya Elimu Duniani ya mwaka 2006 ilikuwa na nembo ya "Kila Mtoto Anahitaji Mwalimu Mmoja", hata hivyo hapa tunapenda kuchukua nafasi kusisitiza kuwa ' Kila mtoto anahitaji mwalimu... ambaye anaendeleza kwa vitendo ujumuishi katika elimu'.

Watoto wanahitaji walimu ambao wanajua jinsi ya kufanya madarasa yao yawe jumuishi na ambao wataweza kuyatambua mahitaji ya wanafunzi wote hata kama ni madarasa yenye wanafunzi wengi yasiyo na zana. Wanahitaji walimu ambao wanamzingatia mtoto katika mikabala yao ya ufundishaji. Na wanahitaji walimu ambao wanatumia zana za kufundishia na kujifunzia ambazo zinasadifu maudhui na kuendana na tofauti zilizomo katika jamii.

Lakini hata hivyo walimu wanahitaji msaada wa kuendelezwa stadi, ujuzi na uzoefu muhimu utakaowanafanya kuwa "walimu-jumuishi". Wanahitaji msaada katika kubuni/kugundua na kufanya mabadiliko. Katika toleo hili la *Kuwezesha Elimu* tunapaswa kuchangiana mawazo na uzoefu kuhusu kuboresha namna ya kuwafunza na kuwasaidia walimu katika mazingira ya elimu-jumuishi.

Aina za Elimu ya Ualimu

Ualimu na Msaada vinaweza kuwa katika hali anuwai, kama wachangiaji wana vyodhihirisha hapa: mafunzo rasmi kabla ya utumishi, kozi ndani ya utumishi, mazoezi maalum ya kufundisha, mipango au programu za elimu ya masafa (kwa njia ya posta/ matandao/ video n.k.), mafunzo maalum ya juu, elimu ya juu, na hasa katika kubadilishana mawazo na uzoefu miongoni mwa walimu wenyewe.

Kupanua Uelewa wa Walimu kuhusu Ujumuishi

Katika mkusanyiko wa makala hizi, tunasikia kuhusu kufundisha walimu juu ya kuwasaidia kikamilifu wanafunzi waliotengwa kama vile walemavu wa kutosikia au wanye vilema vingine. Ambapo elimu-jumuishi ni dhana ya kuboresha namna ya kufundisha makundi yote ya wanafunzi, baadhi ya makala hizi zimejikita zaidi kwenye mafunzo ya walimu katika ujumuishi. Tunapaswa kujiuliza: je dhamira ya ufahamu zaidi kuhusu 'elimu-jumuishi imeshaelezwa kiasi cha kutosha katika programu za mafunzo ya ualimu? Ama, je tunasaidia au kurudisha nyuma dhana nzima ya elimu-jumuishi kuptia mafunzo ya ualimu ambako ujumuishi umehusishwa hasa na ulemavu tu?

Uzoefu dhidi ya Nadharia

Makala nyingi zimeonesha umuhimu wa mafunzo kwa vitendo badalla ya walimu kuhangaikia nadharia tu kwa kuzitafsiri kivitendo. Zaidi ya hayo, walimu wanahitaji msaada wa kutumia uzoefu na ubadilishanaji wa mawazo kuhusu ugunduzi wa kivitendo (ufundishaji) kupitia kazi yao ya ualimu. Hata hivyo ubunifu na ugunduzi wao hujikuta ukisuasua, na hivyo wawape nafasi/msaada kupitia mafunzo na

ubadilishanaji uzoefu. Hapa tumeingiza baadhi ya makala ambayo yanaonesha aina mbalimbali za ugunduzi/ubunifu ambao walimu kawaida kabisa wanaufanya kila siku ambao tunaweza kuutumia katika kuwahamasisha walimu wengine.

Kuchanganyika kwa Walimu

Hapo juu tumeeleza kuwa watoto wanahitaji zana za kujifunza/kujifunzia ambazo zinakidhi tofauti zilizomo katika jamii yao. Vilevile wanahitaji walimu ambao watakidhi tofauti hizi, na ambao watakuwa mifano halisi kwa wanafunzi wanaotengwa. Programu za mafunzo ya Ualimu kama ile iliyoko nchini Msumbiji ambayo inalenga kutoa mafunzo kwa walimu walemavu ni muhimu hapa.

Hali kadhalika masuala ya jinsia na ukabila/ujimbo yanapaswa kufanywa kama hapo juu, ingawa hatukupata makala yoyote inayozungumzia masuala haya. Katika nchi nyingi kuna walimu wa kike wachacha (hususari katika sekondari na elimu ya juu) na huenda wanakabilikwa na vikwazo vya kijamii na kiutamaduni katika ufundishaji wao. Bado kama tunataka usawa wa ujumuisho wa wasichana katika elimu tunatakiwa kuhakikisha kuwa wanawake zaidi wanafunzwa valimu na kusaidiwa, na pia walimu wafundishwa kuboresha usawa wa kijinsia kupitia katika kazi yao.

Katika nchi nyingi, makundi madogo ya kikabila/kijimbo hujikuta yakitengwa au kunyimwa elimu kutokana mara nyingi kikwazo cha lugha. Walimu huenda mara nyingi kutoka katika makundi ya walio wengi katika jamii na hukosa stadi ama ujuzi wa kuwasaidia wanafunzi wa hayo makundi yaliyotengwa, na au hawatika hata kufanya kazi katika maeneo hayo ya vijijini. Walimu watokao katika makundi hayo hawafundishwi kikamilifu. Wanahitaji dozi kamili ya mafunzo au msaada wa zaida kukamilisha mafunzo yao ya ualimu na hasa pale lugha ya kufundishia inapokuwa siyo lugha yao ya nyumbani (ya kikabila). Programu zote zihusuzo mafunzo ya ualimu zinapaswa kuyajua masuala haya yote na kuyashughulikia kama sehemu ya juhudi za kuleta ujumuisho katika elimu.

Kuwasikiliza Wanafunzi

Hatimae, tunagusia jambo muhimu sana ambalo halisisitizwi katika elimu ya ualimu – nalo ni maoni ya wanafunzi. Wanafunzi wa umri wowote wana fursa sawa katika kutusaidia kuboresha Ualimu ukizingatia kuwa wao ndio hukaa muda mwingi na walimu kuliko ule wa wakufunzi au wapanga sera serikalini! Katika kurasa za katikati za toleo hili tutasikia wanafunzi kutoka shule ya Westleigh ya Vingeriza ambao walitumia mradi wa picha kujadili na kueleza mawazo yao kuhusu sifa za mwalimu bora. Je, mawazo yao na ya kwako yanalingana kwa kiasi gani kuhusu sifa za mwalimu bora? Tunaweza kuyatumiaje maoni na mawazo ya wanafunzi kama hawa katika kuboresha mafunzo ya walimu? Wewe katika mazingira au muktadha wako, ungeyatuniaje maoni kama haya ya wanafunzi?

Wanafunzi wa Zambia wakielezea projekti ya picha (EENET)

> "Watu wa hawagundui au kulewa kwamba wanaweza kuwa na walimu kwa miezi ingawa hawaoni jinsi wanavyoongea na watoto, kwa sababu wana dhana potofu kuhusu walimu". (mwanafunzi wa sekondari, Uingeraza)

Walimu wana umuhimu mkubwa katika kuifanya elimu-jumuishi kivitendo. Kama mwelekeo wao na vitendo vyao havitazingatia kanuni za usawa na haki za binadamu, na kama hawatasaidiwa kuwa wabunifu na wenye mabadiliko, basi sera zetu na ahadi zetu kuhusu ujumuishi hazitakamilika.

Lugha na Istilahi

Sote tunashughulikia sana lugha – katika kila nchi mijadala mingi huzungumzia matumizi sahihi ya lugha kuelezea makundi maalum ya wanafunzi. Lugha tuitumiayo huashiria mchakato changmano wa elimu-jumuishi. Katika toleo la 8 la *Kuwezesha Elimu* Roger Slee anakaririwa akisema kuwa elimi-jumuishi ni wazo tata na peru ambalo kuhusu vikwazo/matatizo ya elimu. Hata hivyo katika sehemu nyingi, na hata katika programu za elimu-jumuishi zilizopo, baadhi ya istilahi zingali zinatumika kuashiria mkabala wa kiganga unaosisitiza matatizo ya mwanafunzi mmoja mmoja badala ya kuuangalia upungufu uliopo katika mfumo wa elimu.

Sisi kama wahariri wa toleo hili la 'Kuwezesha Elimu' tusingependa kushurutisha istilahi zilizotumiwa na waandishi humu. Hata hivyo tunatoa changamoto kwa wasomaji na waandishi kufikiria zaidi na kujadili matumizi ya baadhi ya istilahi zilizotumika kuwa istilahi zetu zinaendana na mabadiliko katika utekelezaji utendaji wetu unaendana vilivyo na istilahi nyingi siyo rahisi kubadilisha haraka msamiati/istilahi. Isipokuwakwa kuwa tunaanza kuelewa kuamapana maana ya 'ujumuisho' tunawaasa wasomaji na waandishi wajihusishe kila wakati jinsi lugha kuhusu elimu na ujumuisho vinavyotumiwa katika mazingira yao.

Wazo linaloongelewa

Mafunzo ya Ualimu – ni kikwazo?

J.R.A. Williams

Mafunzo ya Ualimu ni kikwazo kama nyenzo ya yakuleta mabadiliko. Hili limeshabainika katika nchi za kaskazini (Ulaya na Marekani) ambapo mipango ya kuwaendeleza walimu walio kazini inasisitizwa na kuendelezwa, na karibu 60% ya kozi kabla ya kuajiriwa huhusisha mazoezi ya vitendo mashuleni. Bado hata hivyo mashirika ya kimataifa yanaendelea na imani ya mafunzo. Imani hiyo ya 'mafunzo' ndiyo serikali nyingi zinayahimiza mashirika yafanye ili kusadifu katika muundo rasmi. Vile vile inasadifu katika mizunguko ya mradi wenye mtindo wa kibiashara.

Mafunzo kwa ajili ya kuleta mabadiliko hayafanyi kazi – na kwa sababu hiyo modeli ya kiganga kuhusu ulemavu haileti mabadiliko ya sera na utekelezaji kuhusu ulemavu. Imejikita kwa mtu mmoja mmoja – Mwalimu afunzwe na kubadilishwa, badala ya kujikita kwenye mifumo na vitu vinavyoyazunguka mazingira ya shule ambavyo ndivyo vitu vinavyosababisha hali ambayo kwa sasi ndiyo iliyopo madarasani.

Mifumo hii imeendelea hivyo bila mabadiliko yoyote. Bila kuingilia mbinu za ufundishaji na mitaala, mahusiano na mazingira yatarejea kama mwanzoni – yaani kile ambacho walimu walikizoea tangu enzi zao za wanafunzi. Mwanamafunzo/mwanachuo anaweza kufundishwa na kusaidia katika kutumia nadharia mpya, mbinu mpya na namna mpya ya ufundishaji . lakini pale anaporudi shuleni au katika jamii ambayo haina mambo haya mapya, ndani ya mwaka mmoja hujikuta akimezwa na hali halisi, na mwalimu huyo aliyegharimiwa katika mafunzo hayo mapya hujikuta ama akiacha kazi au akirejea na kutumia hali halisi inayomzunguka.

Kama Modeli ya kijamii, ujumuishi lazima ujikite katika ujumla wa mazingira yaliyopo. 'Mafunzo' bila shaka ni kipengele kimojawapo katika mazingira hayo, isipokuwa ili yawe thabiti ni lazima ya husishwe na vipengele vingine katika maisha ya shule. Ni lazima yachochee mabadiliko: na vizuri zaidi shule ihusike katika kuleta mabadiliko hayo katika jamii (kwa sababu watu watayaona mabadiliko hayo), na muhimu zaidi kuhusisha shule katika mipango, utekelezaji na usimamizi.

Walimu mara nyingi husema wanataka kwenda mafunzoni, hususan wanapokabiliwa na changamoto mpya za kuwa "mwalimu-jumuishi". Wanachohitaji ni kutaka kuendana na mabadililiko hayo yanayokuwa yakitarajiwa. Wanayachukulia kuwa ni mafunzo maalum kwa sababu mafunzo ndiyo msingi wa mafanikio yao. Zaidi ya hayo, tumeona kuwa walimu hukuza vipawa vyao vya ujuzi na profeshi siyo tu katika mafunzo, bali zaidi ni kwa kuona walimu wazoefu wanapofundisha, kuongea nao, na kujaribu kutenda wao wenyewe. Ni katika mfumo huu wa mahusiano ambapo vitendo na urejeo wake miongoni mwa walimu hufanya mchakato kamilifu wa mafunzo ya ualimu kwa vitendo. Mfumo huu husaidia kutoa changamoto kwa utamaduni

uliozoeleka, na kukuza fikira za ujumuishi, mazoezi na vitendo. Ili ‘kukubalika’ hata hivyo ni lazima mfumo huu ufanyike katika muktadha wa shule nzima ikiwa nipamoja na wanafunzi, familia zao, wafanyakazi wasio walimu, n.k.

Shirika la ‘Okoa Watoto Uingereza ‘(Save the Children UK) hutumia misingi ya ujumuishi katika ulimwengu wa kiarabu kuboresha maendeleo ya mwalimu na ufanisi wa shule nzima. Mwalimu mmoja wa kike kutoka Morocco (mmoroko) alitaarifu kuwa misingi ya Ujumuishi imemua thiri kwa “kufikiria zaidi kuhusu mazingira ya shuleni”. Imemsaidia pia “kuona mitazamo mipya” katika muktadha wa kuendeleza “ushirika wa wanafunzi, walimu, wazazi, na kaya au familia zao” na “ kuelezea uhalisia wa mkabala wa ujumuishi”.

Jamie Williams ni mshauri wa shirika la Okoa Watoto la Uingereza (Save the Children UK) katika ukanda wa Mashariki ya Kati na Africa Kaskazini kuhusu elimu, malezi ya watoto wadogo na maendeleo.
Mawasiliano:
Save the Children UK
25 Dimishq st.
Mohandeseen
Cairo, Egypt.
Simu: +2023459322
Barua-pepe: j.williams@scuk-mena.com

Haki ya Kujibu

Jamie hutoa mawazomuhimu na yenye changamoto sana. Ku linganisha mafunzo ya ualimu ya hivi sasa na modeli ya kiganga kuhusu ulemavu, na nia ya kuleta mabakiliko ya haraka ya modeli ya kijamii ambayo ndiyo tegemeo.

Shule ni miongoni mwa asasi ngumu kubadilika, na katika elimu ya juu ni ngumu zaidi. Si kusudi letu kukataza mafunzo ya Ualimu-bali ni lazima yafanyiwe mabadiliko kama tutasidia shule kuwa za elimu-jumuishi. Hata hivyo hakuna njia-mkato kwa changamoto hii, ndiyo maana tunakaribisha wasomaji wetu wote kuingia katika mdahalo huu na EENET, na waandishi wa toleo hili, na kwa kila mmoja – kuhusu namna yakuboresha elimu ya ualimu. Tungependa kusikia maoni yako!
Mel Ainscow, University of Manchester

Ndiyo, Nilifanya! Uzoefu wangu Binafsi katika Darasa-Jumuishi

Anne E.N. Musalia

Kwa muda mrefu dhana ya elimu-jumuishi haikuwa na maana kwangu. Nilihisi kuwa ilikuwa kwa walemavu kidogo na kwamba ni shule maalum tu zilizofaa kwa watoto walemavu. Kitamathali, sasa mimi ni mama wa mtoto kiziwi; mfano wa mzazi aliyehangaikia shule kwa mtoto aliyetengywa. Pia mimi ni mtumishi wizara ya Elimu nchini mwangu, Kenya, katika kitengo cha sera na mipango. Mnamo 2004, nilipata udhamini wa kwenda nchini Pakistani kusomea shaheda ya uzamili katika elimu. Ni katika programu hii nilipoona uhalisia wa elimu-jumuishi, kama makala hii inavyoonesha.

Kama sehemu ya mazoezi ya kufundisha, nilipangwa katika darasa la 5 katika moja ya shule jumuishi kubwa za nchini Pakistani. Darasa lilikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi walemavu; ikiwa ni pamoja na watotowatatu wenye mtindio wa akili, mmoja asiyesikia, mmoja asiyeona, na kadhaa wenye matatizo katika kujifunza. Mwanzoni nilishangaa; nani angetarajia kufundisha darasa kama hili? Nilikaa nao kwa majuma mawili nikifanya uchunguzi wangu na kujaribu kufanya uhusiano na wanafunzi. Mwishoni mwa majuma mawili nilikuwa na vipindi sita vya masomo ya jamii ambavyo vyote nilifundisha kuhusu michezo ya Olimpiki.

Nilitumia ubunifu wangu kuandaa mazoezi ya kujifunza. Nilipata wanafunzi wa kushiriki katika makundi, msisitizo ukiwa kwenye umuhimu wa kuheshimiana katika kikundi bila kujalitofauti zao. Hali ilikuwa safi kwani kila mtoto alijitahidi alivyoweza kushiriki na walisaidiana katika mazoezi.

Mazoezi hayo ni kambukumbu yangu muhimu ya miaka 11 katika ualimu wangu. Wanafunzi walichora na kupamba rangi, na kutengeneza vijitabu vya mradi kuhusu Olimpiki. Tulikuwa na lundo la mapicha na vipande vya magazeti vilivyokatwa vinavyohusu Olimpiki. Siku yangu ya mwisho ya mazoezi tulifanya maonesho na kuelezea kazi zetu na kufanya maigizo kuhusu michezo mbalimbali ya Olimpiki. Muda wote huu sikuskumbuka kama kulikuwa na watoto walemavu. Mbinu ya vikundi mchanganyiko ilifana sana kwani kila mtoto alijitahidi kushiriki kadiri ya uwezo wake. Kazi yangu mimi ilikuwa kuwaongoza tu.

Hata hivyo mwalimu wao wa darasa alinidokeza kuwa hakufurahishwa nami kwa kuwashirikisha watoto walemavu kuchangia. Na kwamba wazazi wao wanapendelea watoto wao 'hawa' wasitajwe wala kuulizwa maswali darasani ili wasiumbuke. Mwalimu huyu alifanya nijisikie vibaya kuwa niliwasaliti wazazi na watoto hawa, na hivyo shauku yangu ilipotea kabisa.

Hivi karibuni nilitembelea shule hiyo. Walimu walinikaribisha vizuri. Yule mwalimu wa darasa nililowahi kufundisha alisema, "Tunashukuru kuwa umerudi tena shuleni kwetu, ulitufundisha kuwa 'jumuishi'. Sasa hata watoto walemavu ni washiriki wazuri darasani. Ulipoondoka baada ya mazoezi yako ilikuwa vigumu kuwanyamazisha au kuwatenganisha na wenzao darasani". Alisema pia kuwa hata wazazi wao nao

wamefurahi kwa sababu watoto wao wanajifunza vizuri sawa sawa na wenzao wazima.

Mfano wa kazi ya vikundi katika projekti.

Nikirejea jinsi nilivyo kuwa nafundisha darasani, nashawishika kusema kama Mel Ainscow alivyo sema kuwa walimu wana ujuzi zaidi ya ule wautumiao kila siku. Wanachohitaji ni kusukumwa/ kuelekezwa namna ya kutumia ujuziza wanafunzi wao madarasani. Niligundua kuwa dhana ya ulemavu imo katika vichwa vya wakubwa tu, watoto wao wanafurahia kufanyakazi pamoja na hata kusaidiana wao kwa wao ili mradi tu wasaidiwe vyema. Ni walimu na wapanga-sera kama mimi, ambao wanayafanya mazingira ya kujifunza yawe kikwazo kwa wanafunzi ingawa hii hufanywa kutokana na ufahamu mdogo. Wakufunzi na wapanga-sera wanahitaji fursa ya kutosha kuwasaidia walimu kushiriki na kujifunza kutokana na uzoefu. Kuwamo darasani na kupata uzoefu kwa vitendo ni njia bora zaidi ya kujifunza, kuliko kuzamia nadharia ha matokeo ya utafiti tunayoyasoma katika vitabu.

Nitakaporudi nchini Kenya, na kazini kwanga wizara ya Elimu, nitajivuna kwa kwenda na bendera ikipepea juu “Bendera ya Ujumuishi”. Nilifanya darasani, na ninafahamu sasa kuwa elimu-jumuishi ni halisi.

Anne ni Afisa mwandamizi wa Tathmini na Upimaji katika idara ya Elimu Maalum, Wizara ya Elimu nchini Kenya.
Mawasiliano:
Anne Esendi Ngoda Musalia
P. O. Box 13304-00100
Nairobi
Kenya
Baruapepe: anngomu@yahoo.com

Kuwashirikisha Watoto-wafanyakazi katika Elimu, Yemen

Manal AbdulWahed Shareef AlShureify

Ualimu ni moja ya profesheni zenye changamoto sana. Mafunzo ya ualimu mara nyingi hayana ubora na hujikita kwenye nadharia tu, huku yakiwazuia wanachuo kushiriki katika hali halisi wanayoweza kukumbana nayo madarasani. Kuna pia uhaba wa misaada kwa walimu. Katika makala haya Manal anwaangalia watoto-wafanyakazi nchini Yemen, na namna walimu wanavyoweza kuandaliwa ili kuwasaidia watoto hawa mashuleni.

Vikwazo katika Kujifunza

Yemeni ina viashiria vya chini vya maedelea ya uchumi na jamii. Asilimia 40 ya watu wake wana umri chini ya miaka 18, na mfumo elimu katika nchi hauko thabiti. Ufakiri ni kikwazo kwa watu wengi kushindwa kuwapeleka watoto wao shule na badala yake huwapeleka kufanya kazi ya kipato.

Kiwango cha usajili w a wasichana mashuleni kiko chini sana. Familia nyingi nchini Yemeni husomesha wavullana, wakati wasichana huachwa nyumbani kufanya kazi na kuangalia wadogo zao, na hatimae kuolewa wakiwa bado wadogo. Hivyo Yemeni ina watoto wengi wanaofanya kazi. Matatizo ya watoto wengi sana madarasani, ufundishaji duni wa walimu, kukosa motisho wa elimu, na watoto kukosa msaada kwa wazazi, ni baadhi ya vikwazo au matatizo yaliyomo nchini Yemeni.

Hata hivyo watoto wahaofanya kazi hupaswa kukubaliana na masaa mengi ya kufanya kazi, kazi ngumu na za hatari. Kwa kiwango kikubwa, kazi zao huwanyima fursa ya kuendelea na shule, na wakati mwingine huhatarisha afya zao. Mathalani, watoto wengi hufanya kazi katika magereji ya magari (wakinyanyua vyuma vizito); wengine katika kilimo ambapo wanatumia madawa (chemicals) mbalimbali ya kuulia wadudu, na ambako wakati mwingine hunyanyaswa na kudharauliwa.

Kuwasaidia Walimu kuwa Msaada zaidi kwa hawa Watoto (wafanyakazi)

Mafunzo kwa Vitendo

Katika uzoefu wangu huu ndio muundo bora wa mafuuzo kwani unawapa wanachuo fursa ya kufanya mazoezi na kuhusisha na dharia wanazosoma kwa vitendo.

Kutambua Mahitaji ya kila Mwanafunzi

Ambapo mitaala ya elimu ya musingi nchini Yemeni imejikita kwenye vitendo zaidi ya kukariri maudhui kam ilivyokuwa muongo mmoja uliopita, bado wanafunzi wenye matatizo wanapata msaada kidogo na hivyo kuhitaji msaada wa ziada kwa kurudia masomo waliyokwishajifunza. Kwa kuwa hii ni tiba ya elimu ya ziada ilianzishwa katika kituo cha ‘Watoto wafanyakazi’ miaka miwili iliyopita. Lengo lake ni kuangalia watoto walioandi kishwa katika shule za serikali wasio na huduma wala uwezo na kuwasaidia katika elimu waipatayo shuleni. Aidha inawasaidia walimu kutambulisha wanafunza (pamoja na walemavu). Walimu walianza kufundishwa mahitaji maalum

ya wanafunzi-wafanyakazi, matatizo wanayoyakabili, na mambo mazuri waliyo nayo, na umuhimu wa kuyafanya mazingira ya kujifunzia yawe ya kufurahia kwa watoto wote. Pia iliwa saidiaa walimu kufikiria jinsi ya kuwawezesha watoto- wanao fanya kazi kuwa na mwelekeo chanya wa kusoma shuleni; wapende shule.

Kuhusisha Shule na Maisha Halisi

Katika uzoefu wangu, tatizo kubwa kwa 'ujumuishi(katika elimu) wa watoto wanaofanya kazi ni walimu kutumia njia za ufundishaji ambazo hazihusiani na maisha yao ya kilasiku. Watoto wajapo shuleni huwa wana mengikatika maisha zaidi ya wale wasio fanya kazi. Wanajisikia kuchoka wanapoona shule haihusishi chochotekatika maisha yao, na hatimae huacha shule. Watoto wanaamini kuwa kujifunza shuleni ni kupoteza wakati bure, na walimu hushindwa kudhihirisha kinyume cha fikira zao hizo. Ukosefu mkubwa wa ajira kwa wasomi wengi huzifanya familia nyingi ziamini kwamba kuanza kazi mapema ni bora kuliko kuwapeleka watoto wao shule na kufanya kazi ukubwani.

Walimu walifundishwa jinsi ya kuhusisha mazinfira rasmi ya kishule na yale yasiyo rasmi ya nyumbani ambayo ndiko watoto wanafanya kazi. Walimu walifundishwa namna ya kufnaya uchunguzi wa madarasani na kutumia majadiliano ya vikundi vya eatu wanaohusiana na hawa watoto-wafanyakazi walioko katika shule za serikali. Walimu walifundishwa pia namna ya kuhusisha maisha halisi na shule, na wakahamasishwa kutoa mawazo yao kuhusu kufanikisha mchakato huu.

> Uchunguzi wa madarasani ni mbinu muhimu ya mafunzo . Inawasaidia wakufunzi kutoa kile kilecho kusudiwa kwa walimu. Kurudia masomo kwenye video kuna waidia walimu kuona jinsi walivyoyamudu masoma hayo na kuwawezesha kufikiria majibu na mahitaji ya wanafunzi wao.

Walimu walihamasishwa kutumia uzoefu wa kazi za wanafunzi ili kufanya masomo ya shuleni yahusiane na maisha yao ya kila siku. Kwa mfano katika masomo kama Hisabati walitumia maigizo ya dukani kuuza na kununua vitu na hivyo kufanya somo lisadifu maisha yao. Walitumia stadi za mawasiliano za wanafunzi wanapokuwa katika hasira na kusuluhishana mitaani; lengo likiwa ni kukuza stadi za lugha ya Kiarabu.

Katika mchakato huu mzima watoto- wafanyakazi hawapaswi kupuuzwa. Katika hili wakufunzi wazuri wa walimu ni wanafunzi! Wakipewa nafasi ya kutoa mawazo wataweza kuchangia sana katika kujifuuza kwao na kuwafanya walimu kujua barabara mahitaji yao.

Manal Alshurefy ameteuliwa hivi karibuni kuwa afisa wa programu ya elimu-jumuishi katika shirika la 'Okoa Watoto la Sweden nchini Yemeni.
Mawasiliano:
S.L.P: 18624
Sana'a
Yemen
Barua-pepe: malshureify@scsmena.org

Kuunda upya Mfumo wa Elimu wa Kisovieti, Kyrgyzstan

Chinara Djumagulova

Katika kyrgyzstan udhalilishaji dhidi ya watoto walemavu katika mfumo wa elimu ni kasumba ya Muungano wa Kisovieti. Mfumo huu haukuwa sadifu; uliwaweka watoto walemavu katika shule au asasi za elimu kutegiemeana na aina ya ulemavu waliyokuwa nayo. Mfumo huo wa kutenga watoto ulisababisha watu kutoshirikiana kwa urahisi na uliwanyima watoto walemavuhaki yao ya elimu. Wakati wa kipindi cha mpito baada ya usovieti, kumekuwa na upunguzaji wa idadi ya shule za walemavu Kyrgyzstan kutokana na uhaba wa fedha. Na matokeo yake watoto hao huachwa majumbani bila elimu, ama kuingizwa katika kwa walimu na wanafunzi msaada wowote kutoka kwa walimu na wanafunzi wengine. Mwaka 1998 shirika la Okoa Watoto la Uingereza (scuk) liliombwa kusaidia kutatua tatizo hilo huko Naryn. Katika makala hii Chinara anaelezea jinsi shirika la Okoa Watoto la Uingereza lilivyochukua hatua kuboresha elimu-jumuishi baada ya mfumo wa kisoviet nchini.

Mafunzo ya Walimu Kazini

Kazi kubwa ilikuwa kuwabadili walimu kuhusu watoto walemavu kwa sababu mara nyingi walikuwa wakiwatenganisha na watoto wengine. Zilitakiwa standi na mbinu mpya, na niliandaa moduli zifuatazo:

1. Misingi mikuu, falsafa na dhana ya elimu-jumuishi: kuhamasisha kuwa watoto walemavu wana haki ya kupata elimu na kupewa nafasi sawa katika jamii.
2. kuwaimarisha na kuwaendeleza baadhi ya walimu ambao watatumika kuwafundisha walimu wengine kuhusu utekelezaji wa elimu-jumishi.
3. kutambua na kushughulikia mahitaji/matatizo ya watoto walemuvu katika madarasa-jumuishi kwa kuzingatia mwongozo waUNESCO* moduli hii inawasaidia walimu katika kuelewa na kubainaisha mahitaji ya kila mtoto, kuandaa mimpango maalum kwa kila mtoto, kuyaelewa mazingira halisi ya darasa, kutumia njia shirikishi katika kufundisha watoto wenye ulemavu na uwezo tofauti, na kutumia mbinu za urafiki katika kuunda vikundi darasani.
4. kuondoa vikwazo katika elimu-jumuishi na kuyabadili maisha ya watoto waliokuwa wametengwa. Mwaka 1998 watoto walemavu ndiyo waliokuwa waathirika sana na mfumo huu, lakini tumeone pia watoto wenye matatizo mengine waliotengwa wakikosa elimu kwa sababu mbalimbali. Tangu Januari 2003 tumetoa mafunzo kwa walimu 11 wa shule za kawaida zilizobainishwa kama shule za majaribio za maendeleo (PDS) na shule 84 za za Kyrgyzstan kama sehemu ya mradi unaogharimiwa na USAID.

* UNESCO (2001) Understanding and Responding to Children's Needs in Inclusive Classroom: A teacher's guide, Paris: UNESCO www.unesco.org/education/inclusive.

Kukutana na walimu wengine kwenye semina na kubadilishana uzoefu wa kufundisha walemavu kuliwahammasisha walimu wengi kukubali na kuona wanawajibika kwa watoto hawa na kuamini kuwa wanaweza kuendelea kama watoto wengine. Orodha ndefu ya vipengele maalum ilitolewa kwa kuangalia kazi za walimu wa shule za kawaida. Hii ilitolewa au kuandaliwa kwa ajili ya kufundishia wakufunzi ambao:

- Wanasaidia walimu shuleni kutumia ujuzi na maarifa waliyopata katika mafunzo ya elimu-jumuishi.
- Kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu utekelezaji wa elimu-jumuishi madarasani, kwa walimu na shule ambazo tayari mafunzo kamili ya meshatolewana kukamilishwa.

Mchakato wa mafunzo husaidia walimu kuyakabili matatizo wanayokabiliana nayo. Na huenda tatizo kubwa kabisa ambalo walimu hukabiliwa nalo ni kuondoa tabia ya kuwatenga watoto walemavu katika jamii. Matatizo mengine ni pamoja na mazingira ya shule kutofikika; kukosekana kwa ujuzi na zana au vifaa vya kutambua matatizo na mahitaji ya watoto walemavu mashuleni; ukosefu wa mitaala inayosadifu, njia nzuri za kufundishia, na mifumo ya tathmini kwa viwango mbalimbali; na ukosefu wa jumla wa maamrifa, habari, ujuzi, na uzoefu miongoni mwa walimu na wazazi.

Kuunda upya Mifumo ya Kisoviet

Katika enzi za Ki- Soviet Tume za Elimu ya Tiba (MPC) zilifanaya kazi mara 2-3 kwa mwaka, kwa kuwachunguza watoto wenye mahitaji maalum(walemavu) na kuwapeleka kwenye mashule. Hali hi ilikoma baada ya kuanguka kwa utawala wa Kisoviet. Shirika la ‘Okoa Watoto’ la Uingereza lilianza kusaidia kuunda upya mfumo wa Tune za Elimu na Tiba (TET) na kubadilisha jina, kwa sasa kinaitwa kitengo cha Utaalam na Ushauri katika saikolojia, tiba na elimu(USTE). Kitengo au huduma hii imependekeza kuwa watoto wote wasaidiwe kusoma katika shule za kawaida. Kitengo hicho cha USTE kimebadilisha vigezo vya kuchunguza na kutathmini ili kuwa vya kujamii zaidi badala ya kujikita kwenye tiba tu. Kinatumia mbinu ya ‘urafiki wa wanafunzi’ na dhima yake kubwa ni kutoa ushauri kwa matatizo yote ya maendeleo yakisaikolojia ya watoto.

Kitengo pia kinawasaidia walimu katika mipango yao binafsi ya kujisomea. Matokeo yake, watoto na wazazi wamepewa nafasi kubwa ya kutoa mawazo yao na uamzi kuhusu maendeleo ya shulle na kusoma.

Kutumia 'Kigezo cha Ujumuishi' (Index for Inclusion)

Hatua yetu ya pili ilikuwa kuanzisha kigezo cha Ujumuishi.[†] Lengo lilikuwa kuzifanya shule ziwe jumuishi kwa kuweka kwanza mambo mapya muhimu ya ujumuishi katika mipango ya shule; kama vile kubadilisha sera, mazoezi/matendo mila na utameaduni. Vikundi vya walimuvya kuratibu, wakuu wa shule, wazazi na watoto walishafahamisha katika kila shule ya majaribio. Tunatarajia kuwa kila shule itakuwa na vigezo vyake vya ujumuishi kwa kuzingatia mahitaji yake mahsusi. Zoezi hili litaendelezwa 2006-2007 chini ya udhamini wetu wa USAID. Pia watahudhuria madarasani kuwasaidia watoto kujufunza wenyewe na kuendana na wenzano madarasani.

Mafunzo katika Kiwango cha Chuo Kikuu

Kozi moja kwa ajili ya wanafunzi wa Chuo Kikuu imeshaanzishwa; inaitw 'Misingi na Kanuni za Elimu-Jumuishi'. Mtaala wa kozi za Saikolojia Maalum na Elimu Maalum unatoa pia vipindi vingi kuhusu elimu-jumuishi. Na zaidi ya hayo, kwa walimu katika kozi za mafunzo na kujiendeleza kiprofeshini huko kwenye kituo cha elimu cha Kyrgyz.

Matokeo

- Karibu watoto 500 (walemavu na wenye matatizo ya kujifunza) tayari wanasoma katika shule za kawaida.
- Watoto wot e pamoja na walemavu wanafaidi mahusiano miongoni mwao, na wanashiriki katika shughuli za shule na jamii.
- Watoto wote wananufaika na njia ya kujiamini katika kujifunza
- USTE inawachukua wanafunzi kirafiki na kutoa ushauri wa kitaalam kwa watoto na wazazi.
- Watoto sasa wanatumia mazingira yanayofikika
- Uelewa wa walimu na jamii kuhusu haki za watoto wote umeongezeka sana.

[†] Soma zaidi kuhusu vigezo vya ujumuishi uk.18-19.

Chinara Djumagulova ni mshauri wa elimu-jumuishi katika shirika la Okoa Watoto la Uingereza nchini Kyrgyzstan. Mawasiliano:
27 Logvinenko street
Bishkek
Kyrgyzstan, 720040.
Barua-pepe: chinara@scuk.kg

Tangu mwezi Aprili 2001, Shirikala Okoa Watoto la Uingereza limetekeleza programu ya elimu-jumuishi nihini Uzbekistan, Kyrgyzstan na Tajikistan likisaidiwa na NOVIB. Shabaha za programu ni kukabiliana na ubaguzi na unyanyasaji wa watoto walemavu na familia zao katika Asia ya Kati, kwa kupitia njia mbili, njia ya jamii na maendeleo ya elimu na malezi, na njia ya sheria na mifumo ya maendeleo ya jamii. Chinara alikuw amshauri wa Elimu-jumuishi katika Asai ya kati mwaka 2002 mpaka 2005, na alilisaidia Shirika la Okoa Watoto la Uingereza kuchapisha seti ya miongozo: *Maendeleo ya Elimu-Jumuishi katika Asia ya Kati (2004, katika kiingereza na kirusi).* Mwongozo umejengwa kutokana na uzoefu na matokeo ya kazi ya Shirika la Okoa Watoto La Uingereza ya kuunda modeli ya elimu-jumuishi kwa kuzingatia muktadha wa nchi za Asia ya Kati.

Chinara ni mwanachama wa timu ya uhariri ya shirika la EENET Asia. EENET Asia ni mtandao wa kupashana habari kuhusu elimu-jumuishi katika Asia ya kati, kusini na kusini-mashariki. Shirika hili lina fuata kanuni na njia zile zile zitumiwazao na shirikamama la EENET, na tayari nalo linatoa matoleo na majarida katika kanda yake hiyo. Tazama ukurasa wa habari za kikanda.

Mafunzo ya Elimu-Jumuishi, Papua New Guinea

Frances Gentle

Papua New Guinea ni nchi iliyo katika kisiwa cha bahari ya Pasifiki kusini, ambayo ina idadi ya watu takribani milioni 5 na laki 2. ina misitu minene na maeneo ya milima na swampo au mabwawa ambavyo hivi hufanya usafiri kati ya majimbo yake 20 uwe mgumu sana. Idadi kubwa ya wakazi wake huishi vijijini (mashambani). Mtawanyiko huu umesababisha lugha, utamaduni na mila za zaidi ya makabila 700 na koo zake zidumu kwa miaka dahari. Serikali ya nchi hii imezingatia sana elimu-jumuishi. Imeweka falsafa ya ujumuishi katika sera yake ya elimu maalum (1994) na mpango wake wa taifa wa elimu wa idara ya elimu wa 2004-08. Nchi hii pia ni mshirika la UNESCO kuhusu 'Elimu kwa Wote' ifikapo 2015. maazimio ya elimu-jumuishi huhusisha pia kukuza nguvukazi kwa kutoa mafunzo ya walimu wa elimu maalum, kabla ya utumishi na wakati wa utumishi.

Sensce ya Taifa ya mwaka 1990 nchini PNG ilibainisha takriban watu 12,000 wenye ulemavu, na wote wakiwa naumri wa zaidi ya miaka 10. Idadi ya watoto walemavu walioandikishwa mashuleni haikupatikana kutokana na taifa kutokuwa na utaratibu mahsusi wa kuhifadhi data zilizo kusanywa.

Utoaji wa huduma za elimu maalum katika nchi unaongozwa na serikali kupita kamati ya Elimu maalumu ya taifa na kitengo cha elimu maalum cha taifa. Vituao 14 vya elimu maalum vilivyojengwa katika mijimikubwa na majiji ndivyo hujishughulisha nba utoaji wa huduma za elimu maalum. Vituo hivyo huendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali, yakiwa ni pamoja na Mtandao na huduma wa 'Callan Christian Brothers', Msalaba Mwekundu (Red Cross), na umoja wa Wasioona wa Mtakatifu Yohana (St. John's Assiciation for the Blind). Vituo hivyo husaidia familia na watoto walemavu, walimu na wakuu wa shule, na pia hutoa hudumia za kujiakimu za jamii kwa watoto walemavu ambao hawaendi shule.

Kabla ya mwaka 2004, hakukuwa na programu za shahada ya Elimu Maalum nchini Papua New Guinea. Wanachuo waliokuwa wakimalizia shahada zao za elimu wlikuwa wakichagua kozi moja tu ya elimu-jumuishi kukamilishia shahada zao za Elimu. Mnamo 2004 Chuo Kikuu cha 'World Divine' kikishirikiana na Taasisi ya Masomo ya 'Callan' (Callan Studies Institute) kilianzisha rasmi programu ya shahada ya kwanza ya Elimu Maalum (Bachelors degree). Shabaha na maazimio ya programu hii yanaonekana bayana katika madhumuni ya Mpango wa Elimu Maalum wa Taifa. Madhumuni hayo yalikuwa ni kuendeleza profesheni ya ualimu wa elimu jumuishi kwa kiwango cha chuo kikuu, ikiwa ni pamoja na njia-jumuishi za ufundishaji, miundo yua shule, na uongozi wa shule mbalimbali.

Programu hiyo ya shahada ina vitengo 8 vya elimu ya masafa (distance education), na kila kimoja kikiwa na juma moja la lazima kuwkutanisha wanafunzi husika kwa ajili ya kuchambua au kufundishwa mada au kipengele maalum. Maudhui ya programu ynasisitiza ushirikishwaji wa nguvu au tija za wadau wote kama walimu, walimu

wakuu na watoto wenye ulemavu katika programu. Kwa kuzingatia umuhimu wa utoaji elimu maalum na jumuishi nchini, shahada ya kwanza kabisa ya kitengo cha elimu maalum ilikuwa ya elimu-jumuishi, ambayo ilitolewa kwa mara ya kwanza chuoni hapo katika muhulawa 1, 2004.

Kituo cha Renwick hutoa mihadhara na kusaidia vifaa vya kitaaluma katika kozi za shahada hiyo. Misaada hiyo ni pamoja na utoaji wa miongozo ya masomo, vitabu vya kusoma, zana au vifaa vya ziada, na utoaji wa mihadhara kwenye uniti za elimu-jumuishi na kufundishaji wa watoto wasioona. Maudhui ya unite hizi mbili yanajumuisha mtizamo na msimanio wa kimataifa kuhusu ujumuishi na ulemavu, pamoja na utafiti wa njia bora za kufaa katika nchi zinazoendelea.

Wanafunzi wa programu kwa sasa ni wafanyakazi kutoka vituo vya elimu maalum wakuu wa vyuo, walimu wakuu, na walimu wa darasani wa shule za kawaida. Wengi wa wanafunzi hawa hujigharamia wenyewe, na wote wamedhamiria kuinua kiwango cha elimu-jumuishi katika shule na huduma za jamii.

Kuendelea kwa programu ya Shahada ya kwanza ya Elimu Maalum nchini PNG ni hatua moja mbele katika kutafsiri sera ya elimu maalum kivitendo mashuleni na katika jamii. Ifikapo mwaka 2006 awamu ya kwanza ya wahitimu wa chuo kikuu watarejea mashuleni, vituo vya elimu maalumu, na sehemu mbalimbali za kazini walikotoka nchini. Programu ya shahada ya elimu maalum itakuwa imetoa kundi la wanataaluma wenye maarifa, ujuzi, tabia/mwenendo, na mwelekeo wa kuwa viongozi wa kesho katika uwanja wa elimu maalum, na kuleta mabadiliko katika viwango vya kaya, jamii na taifa kwa jumla. Inatumainiwa kuwa wataleta mabadiliko katika vizazi vilivyopo sasa na vijavyo baadae vya wenye ulemavu nchini Papua New Guinea.

Frances ni mhadhiri wa upofu katika kituo cha Renwich. Mawasiliano:
Renwick College, Royal Institute for Deaf and Blind Children (Chuo cha Renwick, Taasisi ya watoto wasioona na wasiosikia),
361-365 North Rocks Road
North Rocks NSW 2151
Australia
Barua-pepe: frances.gentle@ridbc.org.au
Tovuti: www.rodbc.org.au

Mafunzo ya Ualimu, Uganda

Stackus Okwaput

Makala hii inaelezea uzoefu wa taifa la Uganda katika kuonesha umuhimu wa sera ya taifa na nia ya mafunzo ya kumwandaa mwalimu ili awe mtekelezaji mzuri wa elimu-jumuishi.

Elimu Maalum nchini Uganda ilianza mwaka 1952. Serikali ya kikoloni ilianza kutoa kwa kutenganisha huduma za 'elimu maalum' kwa watoto wachache waliokuwa na matatizo ya kuona, kusikia, kujifunza na mtindio wa ubongo baada ya kuona watoto walemavu walikuwa hawanufaiki na mfumo wa elimu iliyokuwa ikitolewa. Hat hivyo walemaavu bado walibagiliwa kutokana na imani na mwelekeo wa jamii, na hivyo maendeleo ya 'elimu maalum' yalikuwa ya taratibu mno. Elimu-jumuishi imejikuta ikionekana kuw njia ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanashiriki na kupata elimu. Walimu wote wamejikita katika kuutekeleza mkakati huu. Hatua kadhaa zimechukuliwa kuhakikisha kuwa walimu wa Uganda wanakuwa mahiri wa kufundisha watoto walemavu na wale wote wenye matatizo katika kujifunza – katika mazingira –jumuishi. Hata hivyo bado kuna baadhi ya maeneo muhimu ambayo yanatakiwa kuangaliwa zaidi.

Mwanzoni serikali ya Uganda haikuwa na sera kuhusu mafunzo ya ualimu katika elimu maalum. Katika mwaka 1992, serikali ilianzisha sera ya elimu kwa ushirikiano na maendeleo ya taifa, ikinadi kusaidia elimu maalum kwa kufadhili kifedha na kutoa mafunzo ya ualimu. Sheira ya Bunge ya mwaka 1991 ilipitisha Taasisi ya Taifa ya Elimu Maalum(TTEM) (kwa sasa ni kitivo cha Elimu Maalum, Chuo Kikuu cha Kyambongo) kufundisha walimu wa elimu maalum. Hali hii imewezesha Uganda kuanza kuitikia wito wa 'Elimu kwa wote'.

Kitivo kinatoa Astashahada (Certificate), Stashahada (Diploma), na programu za Shahada ya kwanza kwa walimu wengineo, na kimepanga kuanzisha programu ya Shahanda ya Uzamili katika Elimu Maalum. Programu hizi zinawawezesha walimu kupata maarifa, ujuzi na uzoefu muhimu katika kufundisha watu wenye ulemavu na wale wenye matatizo ya kujifunza (k.m. wazazi wangali wadogo kiumri, watoto wa mitaani, watoto wa makundi yaliyotengwa, wale waishio na/ au wenye VVU/UKIMWI na matatizo mengine ya kiafya, wale watokao katika jamii za kuhamahama, watoto yatima, watoto wanajwshi na wale walioathirika kisaikolojia).

Ili kuwafikia walimu wengi zaidi, mafunzo hutolewa kwa kozi ya miaka miwili ya bweni na kozi ya miaka mitatu ya elimu ya masafa (distance education). Kozi zote mbile ni kwa walimu ambao tayari walishasomea ualimu wa kawaida. Kozi hizi zinahusu mikabala yote ya kusaidia makundi mbalimbali ya watoto wenye mahitaji maalum, na kila kozi ina kipengele cha Elimu-jumuishi. Tangu 1990, walimu 716 walishapata mafunzo ya Shahada ya Kwanza na Kozi zo Stashahada (Diploma); na kati ya mwaka 2000 na 2003, walimu 1,451 walijiandikisha kwa Kozi za Elimu ya Masafa (distance education). Hata hivyo idadi hiyo siyo kubwa ukilinganisha na maksio ya walimu 130,000 walioajiriwa katika shule za msingi. Zaidi ya hapo, Kitivo Kikisaidiana na Wizara ya Elimu na Michezo, hutoa mafunzo ya walimu-kazini katika kiwango cha mikoa. Na wengi wa hawa wamekuwa wakiteuliwa kuwa waratibu wa elimu maalum.

Wakati sera hizi zimefanikiwa kuendeleza mafunzo ya walimu – kazini, bado kuna matatizo ya ajira kwa walimu wa Shahada ya Chuo Kikuu ambapo wengi wao huacha kazi na kutafuta kazi kwingineko. Katiba ya nchi inataja haki na fursa sawa za ajira. Mfumo wa serikali za Mitaa nchini Uganda unabainisha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinawajibika kupeleka walimu wake kwenye mafunzo kutegemeana na mahitaji ya wilaya husika, lakini bado ajira ya walimu wenye elimu maalum katika baadhi ya wilaya inategemeana na mwelekeo wa Mamlaka husika. Tunataka mkakati mahsusi uwekwe wa kuhakikisha sera inapitishwa ya kutoa mafunzo ya elimu maalum kwa walimu katika kila shule. Kunatakiwa pia sera ya kuhakikisha kwamba walimu wote mashuleni wanapata mafunzo ya elimu maalum kutoka Chuo Kikuu ama kwenye ngazi za Mikoa ili wawezi kuwasaidia wanafunzi wote katika madarasa-jumuishi.

Matatizo mahsusi ya kujifunza katika kusoma, kuandika na elimu ya hesabu ni moja ya sababu za wanafunzi wa shule za sekondari kuacha masomo nchini Uganda. Kwa hiyo tunaomba ya pitiwe upya mafunzo yanayotolewa kwa walimu wote ili yaweze kuwapa maarifa na ujuzi wa kuweza kusaidia wanafunzi katika maeneo haya pia.

Serikali ya Uganda inaendelea kutafuta misaada kutoka ndani na nje ya nchi ili kuziba mapengo katika mfumo wa mafunzo ya walimu-Kazini na zana toshelevu za kufundishia ili kuboresha mafunzo kwa ajili ya elimu-jumuishi. Kutokana na idadi tuliyoiona hapo juu, bado juhudi za makusudi zinatakiwa kutoa mafunzo haya kwa walimu zaidi(au wote) ili kufanikisha elimu-jumuishi katika ngazi zote za elimu nchini. Matayarisho ya walimu wa elimu-jumuishi yanahitaji sera zinazotekelezeka na pia yanahitaji fedha za kuendesha mafunzo. Aidha kunatakiwa sera ya makusudi kwa mafunzo haya kutolewa kwa walimu wote wa ngazi zote za elimu nchini.

Stackus ni mhadhiri/mkufunzi wa walimu katika Idara ya Elimu Maalum, Chuo Kikuu Kyambongo, na ni mtaalam na mtaaluma katika matatizo ya UZIWI, na elimu-jumuishi.
Mawasiliano:
Faculty of Special Needs and Rehabilitation
Kyambogo University
P.O.Box 1
Kyambogo, Uganda.
Barua-pepe: stackuso@yahoo.co.uk

Kubadilisha Namna Tunavyofundisha, Burkina Faso

Selena Imerovic

Ni njia ipi bora ya kumfundisha asiyesikia? Wengi wanaamini katika mbinu/mkabala-jumuishi kwa kuwaweka pamoja darasani wale wanaosikia na wale wasiosikia. Hili ndilo lilikuwa wazo lililopelekea kuanzishwa kwa Elimu-jumuishi na kituao cha Mafunzo kwa watu wasiosikia na wale wanaosikia mwaka 1988. kituo hiki kilianzishwa na Pastor Kafando jijini Ouagadougou, mji mkuu wa Burkina Faso. Kituo hiki ni moja ya viongozi wa mbinu/mkabala-jumuishi nchini Burkina Faso na kimekuwa na uzoefu wa muda mrefu wa kufundisha wanafunzi wenye na wasio na matatizo ya uziwi tangu ngazi ya chekekea, msingi, na mpaka ngazi ya sekondari. Katika makala hii, Selena anaelezea baadhi ya mbinu au mikabala ya kuhamasisha na kuwasaidia walim kufikiri namna tofauti ya kufundisha na kujifunza.

Kituao hiki kinatumia “Mawasiliano jumla”. Hii inamaanisha kwamba walimu wanawasiliana kwa kutoa maneno na wakati huo huo kutumia lugha ya ishara. Watoto wasiosikia ambao mara chache sana wanakuwa na zana za kusikilizia hupata matatizo sana kuelewa masomo katika kifaransa, ambapo wakati mwingine wanakuwa hata hawana umilisi wa lugha yao ya kwanza, ki-Moore.

Karlet Ouedraogo, mwanafunzi katika darasa-jumuishi anaeleza uzoefu wake:

> “Nina rafiki yangu kutoka shule nyingine ambaye anadhani kungekuwa na sule kwa ajili ya Viziwi tu na kwa ajili yetu tu. Sikubaliani kabisa. Hakuna tofauti baina yetu. Wala sibishani na rafiki yangu Aida asiyesikia, nimajifunza lugha ya ishara, naye anajifunza kusema”.

Hakuna asasi za elimu zinazofundisha walimu wa elimu maalum nchini Burkina Faso. Kituo hicho kiliweka programu ya mafunzo kwa walimu kwa ajili ya programu za elimu maalum na elimu-jumuishi. Mafunzo yake yana modulinne, na hutoa maarifa maalum na ujuzi wa kuandaa na kutekeleza mitaala na mbinu za kufundisha, ikiwa ni pamoja na Saikolojia, mambo-msingi ya usikizi, na usemaji.

Moja ya malengo ya kituo hiki ni kukuza ujuzi wa lugha ya ishara katika jamii nchini kwa kutumia warsha na semina, washiriki wataweza kujifunza tajihia (spelling) ya vidole ishara, maneno makuu, na kufanya mazoezi ya kuzungumza ha watu

wasiosikia. Kozi inatoa msamiati mwingi wa lugha ya ishara, na inazidi kuendelezwa na watumishi wa kituo. Mpaka sasa watu 200 wameshashiriki katika harambee hii na wamechangia sana katika mchakato wa ujumuishi. Mafunzo haya pia hutolewa kwa walimu wa kituo hiki.

Fidel Zouma, mwalimu wa shule ya msingi anasema:

> " Mafunzo yalinisaidia sana mwanzoni mwa kazi yangu ya kufundisha, lakini kwa kuwa kufundisha watoto wasiosikia kunashughulisha sana, tunahitaji mafunzo-endelevu".

Issa Tiendrebeogo, mwalimu wa darasa-jumuishi anaongeza kuwa:

> "Kushirikiana na mwalimu wa wasiosikia kumenisaidia sana. Ufundishaji unatakiwa pia upigwe jeki katika vifaa na zana mbalimbali za mtaala"

Malengo ya muda mrefu ya kituo hiki ni pamoja na kupata elimu bora kwa watoto kwa kuendelea kuboresha mafunzo ya ualimu. Juhudi mpya (iliyoanza Januari 2006) kwa msaada wa shirika la kimataifa lisilo la serikali(international NGO internation service) inapata changamoto ya kushughulikia elimu ya viziwi na elimu-jumuishi katika maeneo mapya matano:

- Kutoa habari kwa walimu kupitia utafiti wa mtandao. Tunasadia watu kuelewa kuwa mafunzo haya ya kwenye mtandao yanaendeleza motisho, shauku, kushiriki na kuleta ugunduzi zaidi wa uboreshaji ujumuishi mashuleni.
- Kutoa mbinu anuwai za elimu ya jadi na aina ya mafunzo inayoshabihiana na moja ya haya yafuataya: stadi za mawasiliano; ushirikiano kivikundi,; kwaminina kujiamini; kuhisi kujumuishwa na kubaguliwa. Hii itasaidia kushiriki katika kujifunza, kushirikiana na kushirikisha madarasa.
- Kuthibiti mazingira ambapo hali nzuri na uwezo wa ubunifu vinaweza kusisitizwa kwa njia za maneno au ishara. Hii itahamasisha mtoto kutumia lugha(kusema) na lugha ya ishara, pia na dhara zingine za kuona na kubuni.
- Kuendeleza programu za ufundishaji na mikakati ambayo itaongeza uwezo wa shule kufundisha kwa ufanisi mada kama za sanaa na michezo, elimu ya afya, haki za binadamu, ikolojiana mazingira, jiinsia, n.k.
- Kutafuta ushiriki wa walimu na wazazi katika shughuli za kila siku kwa lengo la kuwaele wesha kwa kina matatizo ya watoto wao, kutafuta ufumbuzi na kuwahamasisha kushiriki. Kushiriki kwa wazazi kunapaswa kuhakikisha kuwa kujifunza kwa mtoto kunapata msaada hata nyumbani.

Tunapenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha kuchangia na kubadilishana mawazo nasi, na kwa pamoja tutafute ufumbuzi mpya wa kusaidia walimu katika kazi zao za kila siku kuhusu elimu-jumuishi. Ukipende kujua zaidi kuhusu warsha zetu, tafadhali wasiliana nasi. Na kama una mawazo na mapendekezo ya namna tunavyoweza kuboresha kazi yetu, tungependa kuyasikia na kuyapata kutoka kwako!

Warsha za Mafunzo ya Walimu zinazoendeshwa na Kituo.

Warsha za walimu zinaendeshwa kwa wakati bayana (kwa kawaida ni kila baada ya majuma mawili) ingawa bado tunaendelea kuboresha kadiri tunavyokwenda. Kwa kawaida tunaanza na kipindi ambacho kinawasaidia walimu kufanya kazi pamoja katika hali isiyo rasmi kama walioizoea – hii ni njia bora kabisa ya kuzoesha utamaduni wa kubadilishana uzoefu. Tunajaribu pia kuwasaidia walimu kujinasua katika matatizo yanayotokana na mazingira na namna wanavyo fanya kazi ili kuona jinsi ambovyo elimu wangependa ionekane (badada ua kung'ang'ania namna inavyoonekana kwa sasa).

Tunatumia warsha kuwapa walimu mbina mbalimbali (zisizo rasmi) ambazo zinaweza kutumika katika kufundisha/kujifunza (k.m. fungua dimba, chemsha bongo, mazoezi ya jozi au vikundi, maigizo, kutumia picha za taswira na michezo, n.k.). Tunawaambia wajadili wanavyojisikia kama washiriki wa warsha au wanafunzi, na tunawaeleza pia wajadili njia zinazofaa kuwekwa ili warsha iweze kuwanufaisha washiriki. Kisha tunawapa kazi ya kufanya – kuendesha warsha katika madarasa yao juu ya mada mahsusi iliyo katika mataala(kwa mfano Haki za Binadamu). Hii inasaidiakuona jinsi mbinu-shirikishi za kujifunza katika warsha ziavyosadifu na kuyafanya madarasa yao kuwa sehemu-jumuishi za kujifunza.

Warsha yetu pia inajdili kikamilifu mada zifuatazo:

- Namna ya kuhakikisha ushirikiano na kujifunza kwa pamoja katika darasa-shirikikshi
- Namna ya kuepuka kuwa msemaji mkuu darasani.
- Umuhimu wa mbinu/mkabala jumuishi wa mtaala (k.m.umuhimu wa kufundisha sanaa na kazi za kubuni katika masomo yote).
- "Ninaweza kuatawala" (namna ya kuthibiti nidhamu katika madarasa ya wanafunzi 60 au zaidi.
- Umuhimu wa mahusiano yaliyopo kati yao na wazazi.

Selena ni mfanyakazi katika shirika la Huduma ya Kimataifa, anayefanya katika kituo cha Mafunzo na Elimu-jumuishi. Kwa wanaosikia na wasiosikia, Burkina Faso. Mawasiliano:

International Service
B.P.6143, Ouagadougou 01
Burkina Faso , Barua-pepe: sellenai@gmail.com

Mtizamo wa Wanafunzi kuhusu Sifa za Mwalimu Bora, Uingereza

'Westleigh H/S and Technical College' ni shule ya sekondari iliyo Kskazini-Magharibi mwa Uingereza. Kikundi cha wanafunzi 7 wa Westleigh wamekuwa wakifanya kazi kwenye projekti/mradi wa picha –shirikishi. Wamekuwa wakijipiga picha na kuzitumia katika mradi kama njia ya kuvumbua na kubadilishana uzoefu wao katika elimu

Wanafunzi-washiriki katika projekti

Wanafunzi hawa wamekuwa wakishirikiana kazi hii na mwalimu mtaalam shuleni, mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Machester, na mjumba kuto timu ya msaada ya mamlaka ya kujifunza elimu ya mitaani (local education). Wanafunzi washiriki wa projekti hii ni sehemu ya 'kikundi cha malezi' cha shuleni ambacho kiliundwa kusaidia wanafunzi wenye matatizo ya kujifunza na ya kitabia shuleni. Wanafunzi wenye matatizo katika kujifunza hawana nafasi wala kauli ya kueleza uzoefu wao wa elimu na masomo yao, na huwa wako kwenye hatari ya kubaguliwa ama kutengwa kijamii na kielimu. Shule ya Westleigh iliamua kujiingiza katika mradi huu picha kua imani kwamba wanafunzi wanaojitahidi shuleni wanapaswa kuhamasishwa kutoa sauti zao na kuchangia mawazo na maono yao. Walihisi kuwa fikra na maoni ya wanafunzi yanapaswa kutolewa na kuzingatiwa na wafanyakazi shuleni (walimu pia).

Katika kutayarisha projekti yao hii, wanafunzi wa Westleigh kwanza walizitazama picha za wenzao kutoka shule zingine zenye mradi kama huo. Picha moja iliwasisimua na kuwavutia mno. Ilipigwa na mwanafunzi mmoja kutoka shule ya nchini Zambia na kuonesha mwalimu aliyempenda. Picha hiyo iliibua shauku na hamu ya wanafunzi wa Westleigh kuuliza maswali kuhusu namna geni shule za Zambia zilivyo, na wanafunzi wa huko wana uzoefu gani wa shule/kimasomo.

Wanafunzi wa shule ya Westleigh walionesha hamu yao ya kuchangia uzoefu wao kuhusu picha za shuleni kwao na wanafunzi wa nchini Zambia. Picha ya walimu wa Zambia pia iliwavutia kufanya uchunguzi wa nini kinamfanya mwalimu awe mzuri/bora. Moja ya mambo muhimu kabisa ya elimu ambayo wanafunzi hawawa Westleigh walizingatia ilikuwa kufundisha na kujifunza. Kwa kutumia mradi/projekti hii, wamechangia fikra na maoni yao kuhusu mambo yanamfanya mwalimu awe (au asiwe) mzuri /bora.

Katika kujifunza shuleni, wanafunzi huona mambo ambayo walimu huyatarajia kwa wanafunzi wazuri lakini mara zote walimu hawawaulizi wanafunzi nini wanafikiri kinamfanya mwalimu awe bora.

Wanafunzi wana fikra nzito sana kuhusu ufundishaji na kujifunza, na fikra zao hizo zinapaswa kuathiri michakato yote hii miwili (kufundisha na kujifunza). Ufahamu wa wanafunzi kuhusu walimu bora na ufundishaji mzuri una maana sana katika shule yao na katika jamii husika kwa mapana. Maoni na mawazo yao yanapaswa kujumuishwa/kuingizwa katika programu za mafunzo ya ualimu.

Picha iliyopigwa na mwanafunzi wa Ki-Zambia: "Hii ni picha ya kitu kizuri. Nilitaka kuonesha huyu ni mwalimu mzuri... mwalimu ninayempenda".

Maoni ya Wanafunzi na Picha

Ingawa wanafunzi wa Westleigh walieleza mtizamo wao kuwa walimu wazuri wanatakiwa kuwa rafiki (na wa kawaida) kwa wanafunzi, bado walisisitiza umuhimu wa nidhamu na kutotetereka kazini. Wanafunzi hawa walipendekeza kuwa ufundishaji mzuri ni ule unaoshirikisha udhibiti, msaada, ucheshi, masihala na kubadilikabadilika.

Hapa kuna maneno ya wanafunzi wenyewe kuhusu mada hii:

- 'Walimu bora hukusaidia. Wanasaidia kukufanya uendelee na kazi yako na kuipitia nyote'.
- 'Walimu wanapokuwa wamefarahi ni vyema, lakini wanapoanza kusema wakati hutishia wanafunzi na wanafunzi hawapendi. Kuwa rafiki na mcheshi kwa wanafunzi ni muhimu-sana.
- 'Walimu wazuri/bora hawachikuli kila kitu kwa hasira wakati wote'
- 'Ni bora zaidi walimu wakikujua wewe na kazi yako ili wajue ulichofanya na ambacho hukufanya, na hatimae wakusaidie'.

Walimu wazuri /bora daima hukuhimiza kufanya mazoezi, na mnapokubaliana, mnafanya mambo mazuri zaidi. Tunapenda walimu ambao ukiwakoroga kidogo wanachekelea, lakini bado wanashikilia na kuzingatia kazi yao. Baadhi ya walimu hukutaka ufanye mazoezi wakati wote, lakini wengine hukatiza na kuwaruhusu kwenda kwenye kompyuta au kutazama video kwa muda fulani. Mmoja wa walimu tuwapendao hujifanya wakati mwingine kama mwanafunzi. Wakati mwingine huwa mkali, lakini anabadilika na kuwa kawaida tena. Ni mpole na mtulivu badala ya kutawaliwa na makelele kwa wanafunzi

Masasiliano:
Mrs. E Broxton
Westleigh Lane
Leigh, Lancashire
W N 7 SNL, UK
Mrs. Broxton ni mkuu mwandamizi wa Elimu Maalum.

Makala hii ilijumuishwa pamoja na kuhariri wa na Ian Kaplan akishirikiana na wafanyakazi na wanafunzi wa 'Westleigh High School'. Ian ni Mtafiti Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Manchester.
Barua-pepe: ian.kaplan@manchester.ac.uk au wasiliana naye kupitia EENET.

Kujitathmini na Ujumuisho, Bahamas

Betty McDonald

Wanataaluma/Wataalam/Wakufunzi wanazidi kugundua umuhimu wa kuwaingiza wanafunzi wa namna zote katika shula za kawaida. Katika makala hii, Betty McDonald anaonesha namna tathmini-binafsi inauyoweza kuboresha ujumuisho. Anaonesha baadhi ya matokeo ya utafiti wake aliofanya kuhusu wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo , Bahamas.

Bahamas ni moja ya visiwa 700 katika bahari ya Atlantiki kaskazini, na kina idadi ya wakazi 301,790. Serikali yake kuu ni ya kidemokrasia, na ni thabiti; haina 'kodi ya mapato' wala sera ya biashara ya mipaka. Utalii ndio chimbuko lake kubwa la mapato ya taifa. Elimu ni wajibu kuanzia umri wa miaka 5-14 na hutolewa katika shule za serikali na za binafsi.

Tathmini Binafsi ni " Ushirikishwaji wa wanafunzi katika kutambua vigezo na/au kanuni zinazotumika kwa kazi yao na kufanya maamuzi kuhusu jinsi waliuyofikia au kutofikia viwango au vigezo hivyo".[‡]

Kutekeleza tathmini-binafsi, wanafunzi wangu hukaa wawiliwawili na kujadili vigezo na kanuni wanazopaswa kutumia kutolea maamuzi ya kazi zao. Hii inaweza kufanywa katika somo lolote, tangu muziki mpaka Hisabati. Huwa ninawapa mwongozo wa kinachotakiwa na kisichotakiwa. Ninasimamia, kuhamasisha na kupendekeza, lakini sioneshi wala siamrishi.

Wanafunzi mara zote wanasiliana na watalii, hivyo wanaweza kujieleza vizuri. Huniuliza maswali na kutoa mapendekezo kuhusu mchakato mzima wa tathmini, na kishatunafanya majadiliano vikundi. Kupitia hatua zote hizi, ninatoa maelezo ya ziada na tunatengeneza mazingira-jumuishi ambamo kila mwanafunzi anajisikia upendo, heshima na kukubalika darasani. Ninatumika kama mfano huku nikijitahidi kutumia njia shirikishi za kujifunza. Kwa namna hii, wanafunzi huanza kufurahia kubadilishana uzoefu na kutatua matatizo, mambo ambayo ndiyo kiini cha elimu-jumuishi.

Mara wanapokubaliana na vigezo na kanuni za tathmini, jozi moja ya wanafunzi hujadiliana na jozi nyingine; hali hii hurudiwa tena na tena mpaka maafikiana ya darasa zima yanapopatikana. Kisha wanafunxi huanza kuvitumia vigezo hivyo kutathmini kazi zao. Kufanya hivi, huzungumza mmoja mmoja kwa zamu wengine wakisiliza na kutoa maoni yao. Uchunguzi wa darasani na njia za kuangalia na kusikiliza kwa makini bila kuandika chochote yanakuwa ni mambo ya kawaida darasani. Tathmini-binafsi kama hii inaweza kabisa kufanyika uwanjani (michezo), maabara, sehemu za wazi, n.k.

Wanafunzi hujaza fomu mbele ya kazi zao kuonesha sehemu zinazotaka masahihisho ya mtu binafsi. Baada ya zoezi hili, wanaweza kujadiliana miongoni mwao makosa ya kila mmoja na namna ya kuyasahihisha. Hii inaweka msigi wa kuboresha vigezo.

[‡] *Boud, D.(1986) Implementing Stundent Self Assessment, Sydney:HERDSA.*

Kila mwanafunzi anajisikia kushirikishwa katika uamuzi kutokana na kushiriki katika mchakato mzima wa tathmini. Wanaelewa mawazo yao yanathaminiwa kwa yakini. Kushirikiana katika uamuzi kunaboresha pia majukumu na umilikaji ambavyo vyote ni muhimu katika ujumuishi. Tofauti tofauti za utalii katika Bahamas zinashangiliwa zaidi ya kuvumiliwa.

Wanafunzi wasioona na wale wasiosikia hupewa nafasi sawa darasani na kusaidiwa na wenzao wazima darasani, kama vile kurekodi habari fulani au maelezo. Wale walio wazito kujifunza, pia hupewa nafasi sawa darasani na kuendana na wenzao. Mazingira-saidizi humaanisha kuwa hakuna mwanafunzi anayenyanyapaliwa kutokana na 'tofauti' yake darasani. Kanuni zetu za mawasiliano darasani zinawazuia wale wasemaji sana kuwameza wale wakimya, na huwa niko tayari kushauri au hata kuingilia pale inapobidi.

Wanafunzi wanaotoka katika familia zenye misukosuko hujisikia vizuri na kukubalika darasani sawa na wengine, badala ya kujisikia kunyamya sika kama ilivyo katika jamii. Kwa kufanya kazi pamoja kwa msingi wa majadiliano ya mmoja-mmoja huwafanya hata walle wenye matatizo ya titabia warekebike na hatimae kukubalika taratibu darasani. Nitumiapo mbinu zote hizi shirikishi, huniwea rahasi kugundua ulemavu au matatizo ya kila mtoto madarasani.

> Kuweka vigezo na/au kanuni kama kazi ya pamoja na wanafunzi huendeleza na kuimarisha mtandao na mshikamano au ushirikiano ambao ni muhimu sana katika mazingira ya ujumuisho.

Tathmini-binafsi huboresha fikira, uwazi, ubunifu, na uwezo wa kufikiria na kutafakari kwa hoja. Wanafunzi wangu hujadili hadi kufikia maufaka mzuri Mchakato huu husaidia hata wanafunzi wenye uwezo kidogo kuimarika kwa sababu hupata fursa sawa kuchangia uzoefu wao katika mjadala, tofauti na ilivyo katika madarasa ya jadi (yaliyozoeleka huko awali). Vikundi vilivyo taabani hupata jeki kwa vikundi vyenye uwezo katika majadiliano na makubaliano. Wanafunzi hupenda katilia mashaka ubaguzi au utengano. Huondoa tabia hiyo na kuutokomeza ubaguzi darasani, na badala yake huboresha mfumo wa elimu-jumuishi ambao kila mmoja wao ananufaika na masomo.

Dr. Betty McDonald ni profesa katika Chuo kikuu cha The Bahamas ambacho taratibu kinaanzisha 'Tathmini binafsi' kwa kazi. Maeneo yake makuuya Utafiti ni Upimaji wa Elimu, Tathmini, Elimu ya Hisabati, na Takwimu-Tumizi. Amechapisha sana katika majarida ya elimu.
Mawasiliano:
Chuo Kikuu cha The Bahamas
P.O.Box F42766
Freeport
Grand Bahama
Barua-pepe: betmcdee@yahoo.com au betmcdee@hotmail.com

Kuyafanya Mazingira ya Kujifunzia Yavutie zaidi, Palestine

Akram Abualia

Kazi yangu ya awali kama mwalimu ilikuwa katika shule ya Alrashayda karibu na Bahari ya'Dead Sea' nchini Palistine. Ni mbali kutoka Bethlehem kama hakuna huduma ya usafiri wa kwenda shule; hii ni kwa sababu ipo katika eneo la Isreal na kambi za jeshi kabla ya mchakato wa amani kati ya Isreal na Palestina kuanza, elimu ilishughulikiwa na mamlaka ya Isreal. Hakukuruhusiwa kujenga mashule ingawa shule zilizokuwepo palestine zilikuwa zimefurika. Wizara ya Elimu ya mamlaka ya Palestine iliamua mbalimbali kufungua mashule katika sehemu za nchi, kama vile katika nyumba za kupanga, vilabu, na vituo vya umma. Shule yangu ilikuwa moja ya hizi shule mpya katika mskiti na ilinipa changamoto za kutosha.

Hili eneo la jangwa lina mabedui wengi ambao huhamahama kufuatana na hali ya hewa na malisho kwa ajili ya mifugo yao. Hata hivyo watu hawa wanazidi kukaa sehemu moja ya kudumu kwa sababu hali ya hewa ya kisiasa hufanya kusafiri kuwe kwa matatizo. Kwa wale wanaoishi hapa inawawea vigumu – watu mara nyingi ni mafakiri na vifaa vya shule harvitoshelezi mahitaji. Idadi ya wanafunzi wa darasa langu hupungua kadiri kipindi cha kipupwe (winter) kinapozidi baridi –wanafunzi 7 kati ya 14 walifuatana na familia zao kwenda Jericho kwenye joto. Na wale waliobaki walishindwa kujifunza vizuri kutokana na baridi kali.

Rafiki yangu aliniambia nijiuzulu na kurudi Bethlehem; hii ilikuwa sehemu ya dhiki na walidhani nisingeimudu. Nilijua ningekuwa mwalimu bora na sikukusudia kukata tamaa kirahisi.

Darasa la msikitini halikuwa limejengwa vizuri. Kuta hazikuwa zimenakishiwa, milango wazi na madirisha viliruhusu baridi kuingia; sakafu ilikuwa na virakaviraka na hakukuwa na mfumo wa joto wala umeme. Baadhi ya wanafunzoi hawa kuweza kumudu kununua nguo za joto wala viatu. Kwa hiyo japokuwa walikuwa darasani hawakuwa washiriki wazuri katika kujifunza masomo. Hata mimi niliona vigumu kweli kufundisha katika mazingirahaya.

Nilidhamiria kuwa watoto sharti wapate taaluma; kwa nini hali ya kisiasa na kimazingira iwanyime haki yao ya elimu?

Kwa kuwa hatukuweza kuboresha majengo ya shule, mwanzoni hali halisi ilionekana kutowezekana. Hata hivyo siku moja niliamua tuhamishie samani kwenye kona ya darasa. Kisha Wanafunzi walikusanya mbao, wakawasha moto, na kukaa kwa kuuzunguka kama wafanyavyo majumbani kwao. Tuliendelea hivyo na masomo yetu mpaka hali ya hewa ilipokuwa ya joto.

Watoto walipopata joto niliwaambie waimbe nyimbo na kusimulia hadithi kutokana na uzoefu wao. Kisha nilianza kufundisha. Watoto walifurahia zaidi na kujiamini zaidi katika kujibu maswali na kushiriki katika darasa. Wakati wa mapumziko, wao na marafiki wao na kutoka madarasa mengine walitaka kuongea na kutembea tembea

pamoja nami kwa sababu walikuwa wamesikia kuhusu darasa letu. Wanafunzi waliwaeleza wazazi wao, na w alianza kunitembelea shuleni. Baadhi ya wazazi walikuja kunishukuru, lakini wengine walinieleza ninapoteza wakati wangu bure.niliamua kuwaalika wazazi wote na kuwaa mbia kwa nini nilikuwa ninafanya hivyo. Katika darasa langu. Siyo wote waliokuja mkutanoni, ila ulikuwa mkutano mzuri , na wazazi walisema wangeweza kuniletea chochote kurahisisha kazi yangu.

Siku moja waziri wa Elimu na Mkurugenzi wa kurugenzi ya Ualimu walikuja kufungua shule mpya jirani yetu, katika eneo la mamlaka ya wapalestina. Walipenda pia kuzuru shule yetu. Mwalimu Mkuu aliwaomba walimu waandae makaribisho mazuri. Nilibuni programu ambayo ilihusisha baadhi ya familia kujenga mahema kuw ajili ya ugeni huo, kuwaandaa watoto kuzungumza na waziri na kuimba nyimbo za Kibedui, na baadhi walivaa nguo za kimija. Ilikuwa nisikunjema kwa kila mtu. Mkurugenzi aliiona juhudi na mbinu yangu ya kushirikisha watoto na wazazi, na kunialika kwenda kufanya kazi katika programu mpya ya Elimu-jumuishi. Nilikubaliana naye kwa hiari yangu kabisa nikiamini kuwa ningefanya vyema zaidi kwa watoto waliotengwa katika jamii yetu. Hata hivyo ni kazi yangu niliyofanya katika shule ile ambayo ilinifanya nipende sana kufundisha, na ambayo ndiyo inanisukuma katika kazi yangu hii mpya.

Akram Abualia ni mwalimu ambaye kwa sasa anafanya kazi kama Mshauri wa Elimu Maalum katika Wizara ya Elimu, Palestine. Ni mmoja wa wajumbe 36 walioanzisha programu ya Elimu-jumuishi, na sasa anaratibu programu hiyo katika ukanda wa kati na wa Magharibi wa Gaza.
Mawasiliano:
P. O.Box 168
Bethlehem
Palestine
Barua-pepe: akai122@yahoo.com

Kuchambua Vikwazo vya Elimu Vijijini, Chile

Ana Luisa López

"inawezekanaje sisi kama walimu tuwe na mambo mengi yanayofanana, wakati tunaishi katika mataifa tofauti na yaliyo mbali kutoka moja hadi nyingine?"

Mwalimu, Chile Kusini

Watu wengi katika 'ix Region' kusini mwa Chile hutoka katika kundi la kabila la Mapuche. Wameishi huko kwa karne nyingi na kufanikiwa kuendeleza mila zao na lugha ya *Mapudungun*. Wanajivunia kupigana na Wahispaniola na kukataa kutawaliwa nao. Katika maeneo ya vijijini (mashambani) halimbaaya ya maisha inaenda sambamba na matatizo ya kiuchumi na kubaguliwa, na kuna fursa kidogo sana ya watu kushirikiana au kausaidiana. 'IX Region' inakabiliwa na kiwango cha juu kabisa cha ufakiri nchini Chile. Katika makala hii, Ana Luisa anaelezea jinsi yeye na walimu wenzake wa shule ya kijijini walivyotumia vifaa vya EENET kuboresha majadiliano kuhusu ujumuisho, na namna walivyohamasishwa na hadithi kutoka nchini Zambia. Dhana na mbinu zilizotumika kujenga kumbukumbu zilitokana na *Vigezo vya Ujumuisho.*

Katika mwaka 2004 niliamua kwenda kuishi katika kijiji kilicho kusini mwa Chile ili kushirikiana na walimu wa kule katika mchakato wa utafiti wa vitendo. Nilialika walimu 30 na wafanyakazi wa elimu kuchambua vikwazo walivyo kuwa wakikabiliana navyo katika kufundisha, kujifunza na kushiriki. Kwanza niliwapa *vigenzo vya ujumuisho* na uchambuzi wao ulizingatia dhana na mbinu zilizopendekezwa katika muongozo huo.

Nilifanya kazi yangu katika shule ya chekechea, shule ya msingi na shule ya sekondari – na nilishirikisha jumla ya wanafunzi 500. kama mtafiti wa Ki-Hispania, kufanya kazi pamoja na walimu ilikuwa kazi yangu ya kwanza kuikabili kwani tulihitaji mahusiano yaliyojikita kwenye ushirikiano na uaminifu.

Tuliingia kwenye hatua yenye changamoto kweli kweli. Tuliandaa mikutano kadhaa ya siku moja ambapo walimu waliweza kuzungumzia hali inayoikabili shule yao. Tulichangiana mawazo na kufanyakazi kwa pamoja kuyajibu maswali ya wanafunzi wote. Msingi mkubwa wa changamoto hii ulikuwa ni kufanya kazi kwa kushirikiana na

walimu wengine. Niliona mchoro huu kutoka kwenye CD-ROM[§] ya utafiti wa vitendo ya EENET kuwa wa msaada kwangu, kwani ulisaidia walimu kufahamu vizuri mchakato mzima wa kufikiria katika vitendo, na umuhimu wa kufanya kazikwa kushirikiana.

Mduara wa Utafiti wa Vitendo



Pia tuliona mawazo ya mchoro/ramani ya akili kutoka kwenye CD-ROM ni ya msaada. Hii ilitusaidia kujadili kwa undani kuhusu mambo mazuri (chanya) na mambo mabaya (hasa) ya shule yetu. Mdahalo ulikuwa muhimu katika kuchambua vikwazo na matatizo ya utofauti na kuelewa wepi walioathirika kwavyo.

[§] Kujifunza kutokana na tofauti. Mwongozi wa Utafiti kwa Vitendo ili kupata uzoefu wa Elimu-jumuishi inayoendelea - Tazama ukurasa wa machapisho.

Ramani ya Akili kwa kutumia michoro ya mti

Mtiwa walimu wa sekondari. Mizizi: Uhaba wa motisho ni kikwazo muhimu kabisa.
Shina: Mikakati ya awali, na ikiwezekana kujaribu mipya
Matiwi: Vyanzo mbalimbali vya msaada



Mti wa walimu wa chekechea. Mizizi: kushiriki kwa wazazi na kuhimiza elimu ya chekechea na kufanya matumizi mazuri ya walimu shuleni kwa kuzingatia lugha ya Mapudungun fasihi simlizi, na ikolojia.
Shina: mazoezi yaliyopangwa vyema.
Matawi: kutumia vyanzo vilivyopo shuleni.

Mazoezi yaliwasaidia walimu kuzungumzia vikwazo ambavyo wanafunzi wao walikuwa wakikumbana navyo. Walezi wa watoto wa chekechea walieleza maoni yao: walihisi kuwa baadhi ya wazazi hawajui jinsi ya kusaidia watoto wao kielimu. Walezi wa chekechea walikuwa wanapanga vipindi vya mafunzo na programu za mafunzo kwa radio kwa ajili ya kuwaelimisha wazazina wakufunzi. Idadi kubwa ya watoto yatima ilihudhuria shuleni. Wanapata matatizo kufuata ratiba ya darasa na hivyo huhitaji uangalizi wa mtoto mmoja mmoja. Iliamuriwa kuangalia upya majukumu ya walezi na walimu wasaidizi wao, na mzunguko au mpangilio wa majukumu yao ili kuweza kuyakabili mahitaji ya watoto na kuwashirikisha wote madarasani.

Walimu wa shule ya msingi walirejea namna walivyokuwa wakijibu wanafunzi wao kwa masuala ya tabia na mwenendo. Walifikiria mikakati ambayo wangeweza kutumia kupunguza utoro na uchelewaji wa wanafunzi wao. Pia walihisi kuwa wangepata mafunzo zaidi ya jinsi ya kuwashirikisha wanafunzi katika kuelewa sheria za darasani na katika kujifunza kwao kwa kupanga, na mafunzo zaidi katika mikabala ya kushirikisha na kujifunza kwa watoto. Walijajdili suala la kuwa na wanafunzi yatima shuleni, na ukweli kwamba baadhi ya wanafunzi wanalazimika kuishi shule za bweni kwa sababu makwao ni milimani, na ni maili nyingi na barabara mbovu kutoka vijijini. Walimu hawa pika walieleza kuhusu elimu ya wanafunzi walemavu ambao hufundishwa katika kitengo maalum (ambacho ni sehemu ya shule) lakini ambao kwa kawaida huhudhuria katika madarasa ya kawaida. Walimu walielezea shauku yao ya kutaka kujua zaidi kuhusu namna ya kuwasaidia watoto hawa madarasani.

Walimu wa sekondari nao pia walichangia fikira zao na wenzao wa shule ya msingi. Walieleza matatizo yao jinsi ya kuwahamasisha wanafamilia kushiriki katika kujifunza kwa watoto wao. Katika sehemu nyingi lugha mama ya wazazi (au wazazi wa wazazi) ni *Mapudungun* na hivyo hawawezi kuwasiliana kikamilifu katika lugha ya Ki-Hispaniola. Stadi zao za kusoma ziko chini, na hawawezi kuwasaidia watoto wao kuhusu mazoezi ya shuleni. Wakati mwingine hawajiamini kutokana na kutojua kusoma na kuandika, na kwa mantiki' hii hujikuta hawana mwito na elimu. Hali hii ina kwaza san watoto wao katika mchakato mzima wa kujifunzao kwao.

Wanafunzi wengi wa sekondari huko nyuma walisoma kati ka shule za msingi zilizojitenga, ndogo na za mashambani. Wanapofika katika kijiji wanakuwa hawana uzoefu wa taratibu za shule kubwa ya sekondari; k.m. kubadilika kwa walimu, kufurika kwa madarasa, na kupungua kwa ufuatiliwaji wa mwalimu. Aidha wanajikuta wakiishi mbali na familia zao kwa siku za wiki. Wanafunzi hujikuta wakiwa na matarajio kidogo sana ya maisha yao ya baadae au nafasi za masomo ya juu kutokana na matatizo ya kiuchumi. Hawjiamini kuhusu kupata kazi wanapomaliza shule za sekondari.

Walimu wa sekondari walihisi kuwa haya ni mambo yanayosababisha wanafunzi kukosa motisho na kujiamini. Walifikiria jinsi ya kuyakabili masuala haya darasani, na kupanga jinsi ya kuchunguza zaidi mahitaji ya kikundi cha wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao walikariri daraja. Walitaka kuchambua na kuona kama hali ya kutijiamini na motisho mdogo ni mambo yaliyo kuw uahaathiri kujifunza na kufaulu kwao, na kufikiria kama uchambuzi huo ungueweza kusaidia kupata mawazo au mikakati ya u tekelezaji kivitendo.

Hadithi za hamasa kutoka Zambia

Mkusanyiko wa EENET wa maandishi yaliyoandikwa na walimu kutoka Mpika, Zambia, *'Kutafiti Uzoefu Wetu'* ulitusaidia kuona jinsi walimu wawezavyokutafiti matatizo mahsusi yanayowakabili, kuyafikiria na kuyatafutia ufumbuzi. Nilitafsiri baadhi ya uzoefu wao kwa Ki-Hispania, na tulisoma na kujadili maelezo kuhusu: utoro, ushirikiano, kushiriki, msaada wa vijana, mama wa watoto-pevu, na shule-jumuishi. Walimu walijisikia kusonga mbele walipo ya soma na kuyajadili maandishi haya. Walivutiwa sana walipogundua kuwa matatizo mengi yaliyodondolewa na walimu wa nchini Zambia yalikuwapo pia hapa nchini Chile. Hali hii ilitoa changamoto ya nguvu kwa walimu.

" kama waliweza kufanya, nasi tunaweza angalau kujaribu"

Ninapenda kuishukuru EENET kwa kubadilishana uzoefu na maarifa, na kuwasaidia walimu wa Zambia kuchangia uzoefu wao! Ilitudhihirishia kuwa hatuko peke yetu-tunapata 'changamoto ya ujumuisho' sawa na wenzetu wa duniani kote.

Ana Luisa ni mwanafunzi wa shahada ya Udaktari (PhD) katika shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Manchester.
Barua-pepe: Ana.L.Lopez@postgrad.manchester.ac.uk au wasiliana naye kupita anwani ya posta ya EENET

Vigezo vya ujumuisho ni seti ya vifaa vya shule ambavyo huziongoza kupitia mchakato wa maendeleo ya shule-jumuishi. Inasaidia kubainisha vikwazo katika kujifunza na kushiriki, inahamasisha tathmini na upekuzi wa kina wa mazoezi yote ya shuleni, na huwezesha shule kutathmini maendeleo yake kuhusu kuendeleza ujumuishi. EENET inasaidia kueneza uzoefu wa kutumia 'Vigezo' kusini. Seti ya vigezo vya Ujumuisho inawezwa kununuliwa kutoka 'Kituo cha Masomo ya Elimu-Jumuishi, New Redlan, Frenchay Campus, Coldharbour Lane, Bristol BS16 IQU,UK. Tovuti: www.csie.org.uk bie £24.50 ikiwa ni pamoja na p+p(UK).

Mtandao wa Elimu-Jumuishi Nchini Gambia

John Jatta

Ni kwa kutumia ushirikiano na mtandao miongoni mwa watu na asasi mbalimbali, tunaweza kuleta maendeleo kwa watu wote. Mtandao kuhusu elimu-jumuishi unahitaji mabadiliko ya mwelekeo na dhamira ya kushikilia fursa nyingi na changamoto tata tunazokabiliana nazo. Mtandao huu unaweza kuhamasisha ushiriki na juhudi, kuku nguvu kazi, juhudi za pamoja, kubadilisha uzoefu, na mbinu-ndani ya na baina ya jumuiya, mashule, mifumo ya elimu (maalum na ya kawaida), na juhudi za kitaifa na kibara au kikontinenti.

Uzoefu wangu katika mtandao wa Elimu-jumuishi ulianza miaka 20 iliyopita nilipoanza kufanya kazi ya kuandaa shule maalum kwa ajili ya watoto wasiosikia nchini Gambia. Japokuwa sikuwa na mafunzo rasmi kuhusu elimu ya uziwi, niliweza kubainisha mahitaji ya kielimu ya watoto wasiosikia, kuchunguza na kubaini matarajio na matamanio ya wazazi wao na kupitia tena mapendeleo ya walimu ya njia za kuwasiliana. Niliunda kamati ya uongozi wa wafanyakazi waandamizi na timu ya nguvu-kazi ya 'mzazi-mwalimu'. Timu hizi mbili zilifanya kazi kama kamati-saidizi za kushauri, ambazo zilisaidi sana katika kuunda na kutekeleza programu yetu ya kwanza na njia za kufundishia. Tulipitia programu na njia hizo kila mwaka na kuziboresha. Miaka michache iliyofuata tulianzisha huduma ya tiba katika programu ya shule kufanya kazi na watu wasiosikia katika jamii.

Nilianza uchunguzi wa kanuni na misingi ya elimu iliyotumika katika asasi maalum na vituo vya mafunzo katika nchi zilizoendelea na ndani ya Afrika Magharibi. Nilianza kuweka pamoja mpango wa kuendeleza shule na kuanzisha elimu-jumuishi nchini Gambia. Kisha niliwasiliana na wafanyakazi wenzangu wa shule maalum kwa viziwi na wenye mtindio wa ubongo ili kujadili namna tunavyoweza kushirikiana kazi katika kupata msaada kutoka serikalini na mashirika yasiyo ya serikali. Tulikubaliana na kuweka mtandao, na kuanza kusaka msaada wa vyombo vya habari kutusaidia kuhamasisha wananchi kuhusu masuala ya ulemavu na utoaji wa elimu maalum na huduma za tiba.

Nilifanya mawasiliano zaidi na wenzangu na asasi za elimu maalum nchini Senegal, Seirra Leone, Ghana na Nigeria ili kuchangiana uzoefu thabiti. Tulijifunza mengi miongoni mwentu. Pia nili jikuta nikishirikishwa katika shughuli zilizofanywa na mashirika matatu ya kimataifa kuhusu elimu: Jamii ya Jumuiya ya Madola kwa Wasiosikia; Nyenzo /Juhudi kwa Elimu ya Wasiosikia katika Ulimwengu wa tatu ; na Mfuko wa kimataifa wa kikatoliki kuhusu elimu ya wasiosikia. Niliweza kuhudhuria vikao vingi vya kimataifa kuhusu elimu-vikiwa ni pamoja na makongamano, semina na warsha – vyote vikiwa vinaandaliwa na mashirika hayo matatu kuhusu masuala ya elimu kwa mapana. Walimu kutoka Seirre Leona, Sweden, Norway na Uingereza walijiunga na wenzao wa Gambia kuendesha wa rsha za mafunzo kwa wafanyakazi wa shuleni kwangu.

Namna tofauti za kujifunza na fursa tofauti tofauti za mtandao zilipelekea manufaa siyo tu kwa shule ya Mt Yohana ya wasiosikia, bali pia kwa maendeleo ya elimu maalum na utoaji wa huduma za tiba na ushauri nchini Gambia. Kwa mfano, chama cha Wasiosikia nchini (GADHOH) kiliundwa na kusajiliwaq wakati huo. Uchunguzi wa

ulemavu taifa ulifanywa, na matokeo yake yalisaidia maandalizi ya kuundwa kwa sera ya taifa kuhusu 'Elimu Maalum'. Walimu wengi wa elimu maalum walipewa nafasi za kwenda kusoma nch za nje kama matunda ya ushirikiano uliofanyika baina yetu na watu wa mataifa mbalimbali wakati wa matandao wetu. Tunatumaini wanazuoni hawa wataunda msingi wa wakufunzi katika Chuo cha Gambia na katika Chuo Kikuu cha Gambia. Tulifanikiwa pia kupata mirdi ya maendeleo ya miundo-mbinu, misaada ya kiufundi, na ufadhili wa vifaa vya elimu.

Maendeleo yote haya ni matokeo ya juhudi zangu za mawazo mapya, kubadilishana uzoefu na wengine, na kupeana maarifa na ujuzi kupitia shughuli za matandao. Mtandao kama huu ulikuwa wa manufaa kweli kweli, na wale walioshiriki katika mtandao walijikuta katika udugu na urafiki wa kiprofeshini. Kwa hakika, yote haya yaliwezekana kutokana na imani ya mtandao wa kielimu katika kukabiliana na ujinga na umasikini, na kuwezesha ukombozi na ujumuisho wa watu walemavu. Kwa sasa nimeshastaafu lakini najisikia shukurani kwa msaada mkubwa na ushirikiano nilioupata kuto ndani na nje ya nchi ya Gambia kwa kupitia zile shughuli za awali kabisa za mtandao wa Elimu-jumuishi.

Mawasiliano:
John Jatta
P.O. Box 3158
Serrekunda
Barua-pepe: jatta_john@yahoo.co.uk

Kuwapa Mafunzo Walimu Walemavu, Msumbiji

Erik Schurmann

Nchi ya Msumbiji imekuwa na amani tangu mwaka 1992. barabara mpya, kliniki(wodi za wazazi), viwanda na mfumo wa mawasiliano vyote hivyo vimeanzishwa upya badala ya vile vilivyoharibiwa wakati wa vita ya wenyewe kwa wenyewe. Hata hivyo mamilioni ya wakazi wake bado wanaishi maisha ya kifakiri sana. Licha ya maendeleo katika elimu, zaidi ya watoto milioni moja hawasomi shule kwa sababu ya ukosefu wa walimu na majengo ya shule. Ukubwa wa darasa moja una wastani wa wanafunzi 64, na watoto walemavu hawafikiriwi kabisa katika mfumo wa elimu. Erik ni mkuu wa chuo cha ualimu cha Cabo Delgado kilichopo kaskazini mwa Msumbiji, kinaendeshwa na 'Ajuda de Desenvolvimento de Povo para Povo' (ADPP). Hapa anaeleza changamoto yake ya kuwajumuisha wanchuo walemavu chuoni kwake hapo.

Escola de Professores do Futuro (EP) – (Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu) – ni moja ya vyuo saba vinavyoendeshwa na ADPP nchini Msumbiji. Tangu mwaka 1993, walimu 3,000 wamehitimu mafunzo, na kwa sasa zaidi ya wanachuo 2,000 wameandikishwa kwa ajili ya mafunzo ya kuwa walimu wa shule za msingi vijijini. Kozi hii huchukua miaka miwili na nusu. Zaidi ya masomo ya taaluma, wanachuo hufundishwa kazi za jamii:k.m. kuanzisha shule za awali, kuendesha kozi za Elimu ya Watu Wazima, kujenga vyoo, na kukampeni dhidi ya VVU/UKIMWI, malaria na kipindupindu. Katika mwaka wao wa mwisho, wanachuo hufanya mazoezi ya kufundisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya jamii katika shule za vijijini.

EPF Cabo Delgado inashirikiana na shirika la ulemavu (ADEMO) ambalo hutoa mafunzo kwa wanchuo katika ufundishaji wa watoto walemavu. Wanachuo watatu tayari wameshahitimu na kufuzu na sasa wanafanya kazi kama walimu katika mkoa; na waliobakia bado wanaendelea na mafunzo. Wanachuo walemavu wanabor esha mazingira ya kielimu chuono, wanashiriki katika maeneo yote ya programu, na hudhihirisha wazi kuwa elimu ni kwa wote.

Hadithi ya Salimo

Salimo alijiandikisha kama mwanachuo wa ualimu katika EPF mnamo mwaka 2001. Salimo hutumia kiti cha mataili (wheel chair) hivyo njia ziliboreshwa ili kumwezesha kupita kwa urahisi. Wakati wa mazoezi ya kufundisha, salimo alijiweka sawa ili aweze kuandika ubaoni na alitoka nje ya kiti chake na kuanza kutambaa darasani kuwasaidia wanafunzi. Mradi wake wa jumuiya ulikuwa juu ya ujenzi wa Choo.

Walimu-wanachuo hupata fedha (mshahara) wakati wa mwaka wa mazoezi, lakini utawala wa wilaya hauku mpa mishahara hata mmoja, hivyo Salimo alianza kazi ya kufundisha shuleni. Siku moja bila kutarajia kamati ya ukaguzi kutoka wizar a ya Elimu ilizuru shule anapofundisha Salimo ambapo alikuwa anafundisha Baolojia (elimu ya viumbe) kwa wanafunzi wa Daraja la 7. Kamati ya wakaguzi ilivutiwa sana kumwona akitumia njia-shirikishi za kufundisha na kujifunza, alipotumia lundo la mimea mbalimbali aliyoleta darasani. Wakaguzi hao walibaina kuwa walimu wengine walikuwa wakitumia njia za zamani za kufundisha, huku wakiwanakilisha wanafunzi wao kutoka ubaoni. Kamati ilidokezwa kuwa Salimo alikuwa akifanya kazi bila mkataba wala mshahara; hivyo walisawasisha hali hiyo na kutaka alipwe mishahara.

Mwishoni mwa mafunzo yake kwa vitendo, wanafunzi, walimu na mwalimu mkuu walimtaka akimaliza chuo arejee tena shuleni hapo. Mwalimu Salimo alihitimu masomo yake mwaka 2003 na kufuatana na wahitimu wenzake hadi idara ya Elimu ya Mkoa kupata mkataba wa kufundisha. Akiwa anatoka nje ya jengo hilo afisa mmoja alimsimimisha na kusemma kwamba walemavu hawakuwahi kuwa walimu huko awali. Hivyo Salimo alitakiwa arudishe mkataba wa ualimu aliokuwa amepewa. Chama cha walemavu kiliandika barua kwa niaba yake kwenda idar a ya elimu ya mkoa/jimbo. Jibu lao lilikuwa masharti maalum kwa walimu walemavu yalikuwa hayajatolewa.

Kama Mkuu wa Chuo, nilikutana na Mkuu wa Ajira idarani jimboni. Alibishana na kusema kuwa Salimo hakuwa na vyeti feki hata kimoja. Akasema kuwa wasingeweza kumpa masharti maalum ya kazi bwana Salimo. Mimi niliwaeleza kuw Salimo wala hahitaji ‘masharti maalumu! Hatimae bwana Salimo alirejeshewa mkataba wake wa Ualimu na sasa ni mwalimu sahihi katika shule aliyowahi kufanyia mazoezi alipokuwa bado mwanachuo.

Endapo mwelekeo na utamaduni huo vitabadilishwa, tunahitaji mifano halisi kwa vizazi vipya. EPF Cabo Delgado inalenga kuendelea kuelimisha walemavu – kwa msaada w ufdhili kutoka mashirika na watu binafsi – ili kwamba watu wenye ulemavu wanaweza kufanya kazi kama waelimishaji. Ili tufnikishe elimu kwa wote, tunahitaji walimu walioelimishwa ipasavyo kuweza kufundisha vizazi vya kesho.

Mawasiliano: Erik and Salimo
ADPP EPF Cabo Delgado
CP 395 Pemba
Mozambique
Barua-pepe: dnscabo@teledata.mz

Kubadilisha Mfumo na Elimu Mashuleni: Kutumia 'Vigezo vya Ujumuisho' Nchini Afrika Kusini

Petra Engelbrecht, Marietjie Oswald e Chris Forlin

Index for Inclusion (Vigezo vya Ujumuisho) vilitumika katika shule tatu za msingi katika jimbo la Western Cape nchini Afrika Kusini kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili, zikigharimiwa na UNESCO. Hii ilifungua macho ya wanataaluma kuona maana pana ya elimu-jumuishi – kama juhudi ya kuendeleza shule-jumuishi za jamii na kwa ajili ya kubainisha vikwazo katika kujifunza na kushiriki kwa manufaa ya walimu wote na wanafunzi wote. Masomo yaliyosomwa yalihusu uongozi, kushirikisha wazazi na mafunzo kazini (maendeleo ya profesheni).

Vigezo vilisaidia mchakato adilifu wa kufikiria juu ya utamaduni wa shule, sera na utekelezaji wake, na kubainisha na kuelezea vipao-mbele kama sehemu ya mipango ya maendeleo ya shule. Mwanzoni, walimu wengi hawakujua lolote kuhusu "White Paper 6" au tafsiri pana ya elimu-jumuishi. Waliiona elimu-jumuishi kama maalum tu kwa walemavu. Uzoefu wetu sasa umeonesha kuwa elimu-jumuishi inaweza kutekelezwa kwa mchakato wa kujaribu, kurjelea yaliyopita, maendeleo na ushirikiano. Mara baada ya kuhawilishwa katika muktadha wa nchi yetu ya Afrika kusini, Vigezo vya Ujumuisho vilionekana kutoa modeli ya kufaa katika kusaidia maendeleo ya shule-jumuishi zaidi

Dhamira tano zilibainishwa kama vipengele yakinifu kwa maendeleo ya shule zaidi zilizo jumuishi:

- Falsafa ya shule-jumuishi
- Uongozi wa kidemokrasia, miundo, michakato, mila
- Kushirikiana na wadau wote wa elimu
- Kutambua na kuelezea utofauti wa wanafunzi tabia zao
- Kuelezea na kukomesha kudhalilishana mashuleni

Uongozi

Mipangilio ya kijamii na kazi katika kila shule huathriwa na mtindo wa uongozi uliopo. Wakuu wa shule wana dhima muhimu kuhusu namna walimu na watumishi wengine wanavyoandaliwa kuendana na mabadiliko, mitizamo mipya na utendaji. Uongozi na kidemokrasia na wa kukubali mabadiliko unahamasisha ushirikiano katika utatuzi wa matatizo na mabadiliko endelevu. Uongozi wa shule mbili kati ya nyingi ulifanya utekelezaji wa ujumuisho uwe mgumu; ambapo shule ya tatu inapeta tu kwa sababu ya uongozi wa kidemokrasia unaofanywa nw Mkuu wa shule hiyo.

Elimu 'White Paper 6' (Elimu Maalum): Kujenga mfumo wa elimu-jumuishi na mafunzo

Vikwazo katika kujifunza na kushiriki mashuleni nchini Afrika Kusini husababishwa na: dhuluma ya uchumi-jamii, mwelekeo mbaya (hasi) kuhusu tofauti miongoni mwa jamii, mtaala usio kubali mabadiliko, lugha zisizosadifu kutolea elimu (tatizo la lugha ya kufundishia na kujifunzia), mawasiliano yasiyotosheleza, mazingira kutokuwa salama au kutofikika, kutokuwepo kwa huduma za msaada, sera na sheria zisizotosheleza, kuwapuuza na kutowashirikisha wazazi, na walimu na viongozi ambao hawana mafunzo ya kutosha na sadifu. Shule ambazo huko nyuma zilikuwa zimetengwa nchini Afrika Kusini zinakabiliwa na changamoto hizi. Madarasa yaliyofurika, ufakiri wa jamii, na uhaba wa vifaa huwa mzigo kwa walimu ambao haupaswi kupuuzwa; na yote haya ni matokeo ya utekelezaji wa ujumuisho'
Department of National Education, Pretória, 2001

Ushirikishwaji wa Wazazi

'Sheria ya shuleza Afrika Kusuni ya mwaka 1996 inaafikihaki za wazazi kuchangia kadiri iwezekanavyo mchakato wa kujifunza kwa watoto wao. Hata hivyo kulikuwa na u tamaduni wa kutowashirikisha wazazi katika elimu ya watoto wao. *White Paper 6* inasisitiza kwamba kushirkishwa kwa wazazi katika mchakato wa kufundisha na kujifunza ni muhimu sana katika kuboresha kujifunza na maendeleo ya wanafunzi. Kama wazazi watashirikishwa katika elimu ya watoto wao, hata hivyo itabidi waalikwe rasmi, wamotishwe na pia wawezeshwe. Nafasi ya wakuu wa shule hizo mbili ilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa wazazi kushiriki. Mtindo wao wa uongozi wa kiimla ulisababisha mashaka na huzuni; wazazi hawakuwaamini na hawakujisikia kutembelea shule hizo.

Maendeleo Kazini (ya Kiprofeshi)

Timu za uongozi na walimu kutoka katika jamii zilizo kuwa zimetengwa wakati wa nyuma, bado wanang'ang'ania ubinafsi wa kujiendeleza wao wenyewe. Kutokana na mfumo wa ubaguzi wa rangi wa huko nyuma walikuwa hawatambuliki wala kuwa na nguvu mashuleni kwao. Hali hii kwa sasa inahatari sha uendelezlaji na utekelezaji wa mchakato mzima wa ujumuisho katika shule zile mbili zenye uongozi usio wa kidemokrasia.

Makala hii iliandikwa na: Petra Engelbrecht, Mkurugenzi Mwandamizi wa Utafiti, na Marietjei Oswald, wote wawili wa Chuo Kikuu Stellenbosch; Chris Forlin, Taasisi ya Elimu Hong Kong. Utafiti uliofanywa kwa ushirikiano na: Christell de Koker na Michelle Munro, Chuo kikuu cha Stellenbosch: na Leon de Jager na Abri Arendse, Idara ya Elimu Western Cape, Afrika Kusini

Mawasiliano: Petra, Private Bag XI, Matieland, South Africa.
Barua-pepe: peng@sun.ac.za

Kufanya Kazi pamoja na Wazazi Nchini Uganda

Phoebe Katende

Shirika la 'Sight Savers International' (SSI) linafanya kazi kwa kushirikiana na serikali ya Uganda kuhakikisha kuwa watoto wasioona na wale wenye matatizo ya macho wanapata elimu kuitia mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wote (UPE) katika kila wilaya. Baadhi ya masomo yamekuwa yakisomwa kuhusu kushirikisha wazazi katika elimu ya watoto wao kama Phoebe anavyoeleza katika makala hii.

Mafanikio ya elimu ya mtoto hutegenea kwa kiasi kikubwa msaada wa wazazi au walezi wake. Kuna haja ya kuwepo mahusiano mazuir kati ya walimu, wazazi na wanafunzi. Na hii ni muhimu sana kwa watoto wenye ulemavu. Wazazi wengi wa watoto wasioona na wale wenye matatizo ya macho hawanauhakika na uwezo wa watoto wao. Wazazi wanaweza kuogopa kuwapeleka watoto wao shule kwa kuhofia kuwa wanaweza kupotea, kugongwa na gari, n.k. Watoto wasioona ha wale wenye matitizoya macho mara nyingi huacha shule au huenda shule mara chache tu. Mara nyingi tunawaona majumbani kwao wakifanya shughuli za nyumbani tu, na wakati mwingine wamekaa bure tu.

Dhima ya Vyama vya Walemavu

Wazazi wengi hawafahamu haki za watoto wao kuhusu elimu. Chama cha wasioona cha wilaya ya Kamuli kinawahamasisha wazazi kuchukua nafasi kubwa katika elimu ya watoto wao, na hususan kupitia zaira mashuleni na kuonana na walimu.

Kuwatoa Wazazi Woga wa Shule

Wazazi wengi huenda hawakuwahi kwenda shule enzi zao na hivyo hawana habari na mchakato wa elimu. Shule zinapaswa kuwa karimu na msaada kwa wazazi wanaoonesha mapenzi ya kuzitembelea. Kuhamasisha maendeleo ya vikundi vya msaada vya wazazi ni njia nzuri ya kuwajengea wazazi moyo wa kujiamini na kuwasaidia kuelewa na kujadili maoni ya walimu kuhusu watoto wao. Vikundi vyo wazazi visivyo rasmi vimesaidia kuboresha hali ya wazazi kat ika shule moja wilayani kamuli. Mwalimu mmoja (asiyeona) alisema kwamba wanafunzi wachache wanaacha shule tofauti na zamani, na wengi wao sasa wanazungumza kuhusu wazazi wao kutembelea shule.

Kuwahamasisha Wazazi Kuja Shuleni

Wazazi wanahamasishwa kuwatembelea watoto wao shuleni na kujenga uhusiano wa karibu na walimu. Katika ziara hizi wazazi wataona mambo ambayo watoto wengine hupata shule, na kuona kama yanalingana na yale watoto wao walemavu hupata. Kwa kuliona hili, wazazi wanaweza kuchukua nafasi thabiti katika kuangalia na kufuatilia maendeleo ya watoto wao, na hat kushawishi kupatikana kwa karatasi za 'Breili', mitihani inayofaa, na vitabu vikubwa vya kuprinti. Wazazi wataweza kuongea na watoto wasio walemavu na kuwahamasisha kuwasaidia watoto wa sioona na wenye matatizo ya kuona wawapo madarasani. Mara nyingi wahusika wa masuala haya hujitahidi kupigania haki za watoto hawa bila hata kuhusisha wazazi, ingawa wazazi wakielimishwa na kufahamu masuala haya wanaweza kuwa msaada mkubwa kwa maendeleo ya watoto wao kielimu.

Tumeona kuwa wazazi wanaojihusisha na shule, huwa wanahimiza hata ubora wa elimu katika ngazi ya shule na wilaya ambapo wanonesha uzoefu wao katika shule kuelezea madarasa yao. Mmoja wa wazazi hao aliwahi kumtembelea afisa mmoja wilayani na kumwelezea kuwa “alikuwa mkimya na muelewa tofauti na nilivyo kuwa nafikiri. Hakuna na wazo kuhusu watoto wasioona, na aliahidi kusaidia”. Mzazi huyu alifurahia ziara yake; ilionesha hatua moja mbele.

Nafasi ya Mwalimu

Tunatakia pia kuhakikisha kuwa walimu wana mwelekeo chanya kuhusu watoto walemavu, na wako tayari kushirikiana na wazazi. Walimu wanaweza kusaidia wazazi kwa kuanzisha mpango wa kazi kwa ziara zao shuleni, na wazazi kuhakikisha kuwa walimu wahusika wanakuwepo shuleni wakati wa ziara zao. Wafanyakazi wa jumuiya (kama wapo) wanaweza pia kupewa mafunzo kuwaelezea wazazi nafasi yao katika elimu ya watoto wao.

Katika uzoefu wetu, walimu huwatembelea watoto walemavu makwao na kuwaeleza wazazi wao nini wategemee kwa watoto wao wanaposoma shule, na nafasi yao wao kama wazazi. Mwalimu anakuwa ndiye wa kwanza kumshawishi mzazi awe anatembelea shule kumwona mtoto wake.

Kazi ya Shirika la SSI nchini Uganda imeonesha umuhimu wa kuthamini nafasi ya wazazi katika elimu. Wazazi pia hunufaika na elimu ya watoto wao, na wanaweza kudhamiria kwa dhati kabisa kuboresha haki ya watoto ya elimu hata zaidi ya wataalam ambao wao huona kama ni sehemu ya kazi yao tu na siyo suala la usalama wa familia na furaha. Tunashauri programu zote za elimu-jumuishi zithamini na kutumia nafasi ya wazazi na walezi katika elimu kama lengo ni kupata matokeo mazuri kwa wanafunzi wote.

Phoebe ni Afisa wa Projekti, anayesaidia wakala wa shirika la SSI kuanzisha programu za kuboresha haki na ubora wa maisha ya wasioona na wenye matatizo ya macho, na kuzuia upofu.

Mawasiliano:
Sight Savers International
East African Development Bank Building 2nd Floor, 4Nile Avenue
P.O.Box 21249, Kampala.
Barua-pepe: pkatende@sightsavers.org.ug

Kuzingatia Sera: Iran

Abolfazi Saeedi

Elimu Maalum nchini Oran ilianza mwaka 1941 katika shule ya huruma kwa ajili ya watoto wasiona huko Tabriz. Miaka 3 baadaya, elimu ya wasiosikia ilianzishwa na mwalimu binafsi wa Ki-Iran. Mnamo mwaka 1968 mpango rasmi wa elimu maalum ulianzishwa na shirika la Elimu kwa watoto maaku na wanafunzi katika wizara ya Elimu. Baada ya mapinduzi ya Kiislam (mwaka 1979) Elimu Maalum ilipanuliwa zaidi. Mwaka 1990 shirika la Elimu Maalum (SEM) lilianzishwa. Elimu-jumuishi ilianzishwa mara ilipogundulika kuwa kutenga elimu maalum kivyake hakukuwa kunawezesha elimu hiyo iwafikire wanafunzi wote.

Ingawa idadi ya wanafunzi wasiojiweza katika elimu (chekechea/awali, msingi na sekondari) ilikuwa mara 3 na nusu katika mwaka 2004 zaidi ya mwaka 1990, bado wanafunzi walemavu walikuwa asilimia 0.49 ya wote. Wanafunzi walemavu mijini walionekana kunufaika na elimu maalum kuliko wale waliokuwa Vijijini. Wale wote wenye ulemavu walikuwa hawaoneshwi katika takwimu za taifa, walimuwawanaandikishwa katika shule za kawaida lakini bila kusaidiwa wala kupewa elimu maalum.

Katika mwaka 1999 maafisa na viongozi wa SEM na Naibu wa Elimu ya Msingi wa Tahran walikutana washauri kutoka UNESCO Paris katika warsha kuhusu ujumuisho. Mwaka 2000 kikundi cha viongozi wa elimu kutoka elimu maalum na elimu ya kawaida walitembelea shule za elimu-jumuishi nchini Uingereza, na washauri wa UNESCO walichambua hali ya elimu maalum katika Iran. Mpango wa majaribio wa ujumuisho ulitekelezwa katika majimbo ya Es fahan na Gilan. Warsha 2 zaidi kuhusu mpango wa elimu kuhusu ujumuisho zilifanya mwaka 2002-03 kwa msaada wa UNICEF.

Kuanzia mwaka 2001, uchambuzi kwa ajili ya mafunzo ya walimu, wafanyakazi wa shuleni wasio walimu, maafisa na viongozi wa idara za elimu maalum na elimu ya kawaida. Vitengo viwili vya UNESCO- 'kuyaelewa na kuyashughulikia Mahitaji maalumu ya watoto katika madarasa-jumuishi' na 'Jalada la wazira kuhusu Elimu-jumuishi: Vifaa vya Msaada kwa Mameneja na Watawala' – vilitafsiri kwa Ki-Farsi. Vyote viwili vilikamilishwa na makala kuhusu sababu za kuanzisha mfumo wa Elimu-jumuishi nchini Iran, na filamu za elimu kuhusu ujumuisho nchini Iran na nchi nyingine.

Mwaka 2002, majaribio yaliyofanyika katika majimbo yale mawili yalilifanyiwa tathmini. Programu kwa ajili ya kuendeleza elimu-jumuishi kitaifa iliandaliwa na kuwasilishwa katika kongamano la UNESCO lililofanyika nchini Pakistan mwaka 2003. kutokana na matokeo ya tathmini, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kilionekana ni kitu muhimu katika ufanisi wa programu. Tangu mwaka 2002 idadi ya kozi imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Kwa jumla, walimu 5,788, ambapo kati yao, 3,505 ni walimu kutoka shule za kawaida na shule maalum na 340 ni maafisa na watawala wa Elimu Maalum, wameshapewa mafunzo Semina pia zilifanywa kuwahamasisha maafisa na watawala wa idara za elimu katika ngazi ya majimbo/mikoa. Kozi za

mafunzo kuhusu mipango ya elimu kwa shule-jumuishi zimeshapangwa kwa ajili ya watumishi wa majimboni kati ya 2006-08.

Mwaka 2004, majaribio yali tathminiwa tena na sheria ndogo ikatungwa (kwa kushirikiana na wakurugenzi wa wizara) ambayo inapitiwa na Baraza la juu la Elimu Sheria ndogo hii ilitokana na tathmini, na ilikusudiwa kutoa wataalam zaidi katika shule za kawaida na kuweka sheria kamili ya kuwawezesha watoto walemavu kunufaika na elimu itolewayo katika shule za kawaida.

Kutokana na kuongezeka kwa watoto wanaofaulu mwaka mmoja wa elimu ya awali (umri wa miaka 6), Shirika la Elimu Maalum, Wizara ya Afya na Elimu ya Tiba, Shirika la Ustawi wa jamii, Chuo Kikuu cha Ustawi wa Sayanzi na Taasisi ya Uchunguzi wa watoto Maalum, yako yanashughulikia urasimi wa 'dodoso za umri na hatua'. Dodoo hii inahusu ujazwaji wa wazazi na uangalizi wa mtoto; mfumo ambao unaobainisha watoto wenye mahitaji maalum katika ngazi ya elimu ya awali ili kuweza kuwaelimisha katika umri mdogo na kuwapa nafasi ya kuzoea shule za kawaida. Idara ya Mipango ya Elimu ya Shirika la Elimu Maalum inakusudia kupanua elimu ya awali kwa watoto wa miaka 2-4.

Kufuatana na msaada wa SEM, vyama kadhaa vya wazazi wa watoto walemavu vimeanzishwa. Vyama hivi vinasaidia kutetea haki za watoto walemavu na kukuza ujumuisho mashuleni. Inatumainiwa kuwa vyama kama hivi vitaimarika na kupanua shughuli zake katika muda mfupi ujao.

Juhudi zinafanyika kukuza uelelwa wa jamii kuhusu ujumuisho. Hii inafanyika kwa kutumia masaili ya radio na majadiliano, na filamu za kielimu kwenye Televisheni ya taifa. Mamia ya masali na taarifa za habari yameshachapishwa kwenye majarida na magazeti nchi nzima(Irani). Pamoja na programu ya mafunzo, hamasa hizi zimesaidia kuongeza idadi ya watoto walemavu katika shule za kawaida. Kwenye warsha ya mwaka 2003, Wizara ya Elimu ilibadilishana uzoefu na walimu na maafisa wa kutoka Afghanistan kwa kushirikiana na shirika la Elimu ya Kiislam, Sanyasi na Utamaduni.

Mawasiliano:
Abolfazi Saeedi
Research Institute of Exceptional Children,
36, 5th building of Ministry of Education,
Martyred Moazffar Brothers,
Enghelab Avenue, Tehran, 1416935671, I.R.Iran.
Barua-pepe: aseedi3121341@yahoo.com

Habari za Kikanda

Ásia

Shirika la EENET Asia – Mtandao wa kuwezesha elimu kwa Kanda ya Asia ya Kati, Kusini, na Kusimi-Mashariki – lilichapisha toleo lake la kwanza mwezi Julai 2005. toleo lake la pili bado linachapishwa na kutawanywa, na linaangalia baadhi ya masuala ambayo yalijadiliwa wakati wa kongamano la kimataifa lilileondeshwa na mtandao nchini Indonesia mwezi Septemba 2005. pia linajumuisha mada za: elimu katika makambi; kazi kwa watoto; VVU na UKIMWI, Upatikanaji, na mafanikio ya ujumuisho katika shughuli na mazoezi mashuleni na katika jamii.

Timu ya uhariri ya EENET Asia inakaribisha maoni kuhusu dhamira za toleo lijalo. Kama kuna mada au suala ambalo ungependa litokwe na Toleo la Asia kwa kina, tafadhali wasiliana na timu hii ya uhariri. Baadhi ya masuala ambayo hususan yangeandikiwa makala ni pamajo na:

- Mahusiano baina ya dini na haki za watoto katika elimu.
- Maendeleo ya mbinu ya ‘shule-rafiki wa mtoto’ katika nchi mbalimbali
- Haki za elimu na ujumuisho kwa mtizamo wa wazazi
- Programu za elimu rasmi na isiyo rasmi, na jinsi zinaweza kuhusiana.
- Elimu kwa jumulia zilizonyanyasika(kutengwa), na watoto wanaoishi katika matatizo ya migogoro, baada ya ghasia, au uhamishoni.

Kuendesha Mtandao wa Kikanda Kunafanyikaje?

Tuliiomba timu ya EENET Asia kueleza uzoefu wao kuhusu mwaka wa kwanza walioendesha mtandao.
Anupam Ahuja alieleza:

“Kazi hii kwa kweli ni kubwa na inashughulisha (kwa mkazo!). Jana ilikuwa siku moja tu kati ya miezi yote 3 iliyopita ambayo sikuandika chochote katika toleo letu la pilila EENET Asia. Kuna mengi sana ya kufanya..... kuwandikia watu, kubadilishana maoni, kuwahamasisha waandike, kufuatilia, kuhariri makala, kuchangia fikira zangu na wahariri wenzangu katika timu (ambao hushughulikia nchi nyingine ndani ya kanda), kukubaliana au kutokukubaliakana, kupokea mchango wa mawazo, kutafakari yalopita..... na kila mara kufikiria yajayo. Na sasa naelewa kwa nini Susie (wa EENET – dunia) alisema, nilipoongea naye mwaka 2000, kwamba EENET huchukua miezi 9 kufnikiwa kuchapisha toleo moja... kwa kweli ni MCHAKATO!!”.

Matoleo ya EENET Asia yanapatikana katika printi, 'Braille' na ki – electroniki, na haata katika lugha mbalimbali(k.m. Ki-Bahasa Indonesia, Kirusi na Ki-Urda Kutafuta jinsi ya kupata nakala, tumia barua-pepe: asia@eenet.org.uk au andika kwa: EENET Asia & IDP office, Universitas Sebelas Maret, Jl. Ir. Sutami 36 A, Surakarta, Jawa Tengah, Indonesia.
Pia unaweza kupata kwenye tovuti ya EENET.

Warsha ya Kikanda kwa Asia ya Kusini
Shirika la EENET Asia linahusishwa katika kuandaa warsha za kikanda za UNESCO kwa washiriki kutoka Afghanistan, Bangladesh, Bhutan, India, Maldives, Nepal, Pakistan na Sri Lanka. Warsha ambayo huwa inazingatia maendeleo ya ujumuisho na urafiki-wa-mtoto kielimu chini ya mwavuli wa 'Elimu kwa Wote' itafanyika mwishoni mwa Novemba 2006, jijini New Delhi nchini India.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Johan Lindeberg, UNESCO Bangkoki, P.O.Box 967, Prakhanongo Post Office,
Bangkok 10110, Thailand.
Barua-pepe: j.lindeberg@unescobkk.org

Pacifiki

Majadiliano yanaendelea kuhusu kuanzisha mtandao wa mtindo wa EENET kwa kanda ya Pasifiki. Kama utapenda kujiunga na mtandao huu, au hata kusaidia kufadhili eneo au sehemu ya kuendeshea mtandao, tafadhali wasiliana na Donna Lene, Inclusive Education Co-ordinator (Pride, Samoa) P.O.Box 981, Apia, Samoa. Barua-pepe: donna@samoa.ws

Tafsiri

Shirika la EENET linahitaji msaada wako! Ukweli tunapenda kutoa toleo hili (na mati ni zingine za elimu-jumuishini) katika kugha mbalimbali ili wasomaji wengi waweze kusoma. Hatuwezi kumudu kuwalipa wafasiri, lakini ukijitolea kutufsiri toleo moja au hata makala moja au mbili) katika kugha nyingine, tungependa kusikia kutoka kwako.

Masaili ya EENET

Mnamo februari 2006, shirika la 'Atllllas Alliance' liliendesha warsha ya siku 4 kuhusu elimu-jumuishi huko Zanziba, Afrika Mashariki. Wengi wa washiriki 45 walikuwa kutoka katika mushirika yake wanchama na washirika wake wanaofanya kazi katika ukanda wa Mashiriki na Kusini mwa Afrika, Nepal na Palestina. Warsha hiyo ilisaidia sana washiriki kubadilishana uzoefu na kujifunza miongoni mwao. Mazoezi-shirikishi ya namna mbalimbali yalitumiwa, ikiwa ni pamoja na usomaji wa picha (photo elicitation) – yaani kutumia picha katika kuchochea kumbukumbu za ya tunayofanya katika mchakato mzima wa elimu –jumuishi. Mshiriki mmoja asiyeona Bwana Zefania Kalumuna alihojiwa na Ingrid Lewis wa shirika la EENET kuhusu usomaji wa picha.

Wewe unafikiria nini kuhusu matumizi ya picha kuchochea majadiliano miongoni mwa washiriki wanaoona na wale wasioona?
Mimi nafikiri ni njia nzuri. Ni muhimu kukumbuka nafasi ambayo picha zinazoonekana zinaweza kufanya na zinapaswa kuwezesha mchakato wa kujifunza kwa kila mmoja, ikiwa ni pamoja na watu wasioona.

Ni njipi zipi kikundi chako mlitumia ili kukupa nafasi ya kushiriki katika mazoezi?
Niliona ufumbuzi mzuri ni kuwa na angalau watu watu wawili kunielezea kuhusu picha, ha hivyo ninaweza kukusanya mawazo mengi kuhusu nini kinatokea katika picha. Hivi ndivyo ilivyokuwa tulipofanya uchunguzi wa darasani wakati wa ziara ya mashuleni. Ilikuwa inapendeza kama watu wawili walinifafanulia darasa (mmoja mwenyeji na mwingine mgeni).

Je Kila mmoja alielezea picha kwa namna moja?
Hapana! Mtu mmoja anazingatia kitu kimoja na mwenzake anataja kitu kingine kwenye picha. Kila mtu alikuwa na wazo tofauti kuhusu vikwazo vya ujumuisho vilivyaooneshwa na picha hizo. Niliyale waliyokuwa wakielezea, ya nikizingatia maoni mbalimbali.

Kulitokea nini pale kikundi chako kilipojadili na kuchambua picha?
Niliweza kupendekeza fikira zangu kwa kuzingatia maelezo yao. Wakati mwingine fikira zangu kuhusu tatizo au kikwazo nilichobaini (sababu na matokeo yake) kilikuwa sawasawa ha kile kilichobainishwa na washiriki wanaoona; na wakati niliweza kupendekeza mambo ambayo wao hawakuwa nayo kichwani.

Una maoni gani kuhusu kunufaika na zoezi hili wewe binafsi na washiriki wenzako wanaoona?
Kwa kweli sote tulinufaika na zoezi hili. Ilikuwa vigumu kwangu kutumia zoezi hili, lakini niliweza kufikiria mambo mengi yanayotokea shuleni kutokana na picha. Washiriki wanaoona walinufaika sana kwa sababu wao waliona kwa karibu zaidi picha, kitu kilichokuwa kikiwafanya wachambue hali ya ujumuisho au utengano kwa urahisi zaidi kutokana na picha.

Je zoezi hili linahusiana sana na Elimu-Jumuishi?
Bila shaka! Watoto wasioona wanapokuwa wanajifunza kusoma shuleni wanaweza kuwa na vitabu vya 'braille' ambavyo vina maneno, lakini watoto wenzao wanaoona huwa wana vitabu vyenye maneno na mapicha, hususan darasa la 1 na la 2 vitabu vyao na mapicha karibu asilimia 75. Hii humaanisha kuwa mtoto mwenye kitabu cha 'braille' anakosa mengi sana. Wanaweza kuwa katika darasa moja, lakini wanatenganishwa kwa vitabu tofauti.

Wewe unapendekeza ufumbuzi gani?
Eu trabalhei num projecto que consistia na transcrição de livros de crianças para Mimi nimewahi kufanya kazi katika projekti moja inayotafsiri vitabu vya watoto katika nukuuza 'Braille' na kuna ufumbuzi wa namna nyingi niliojifunza. Kwa kweli, watoto wanoona na wasioona inapaswa wasaidiwe kusoma pamoja ili wale wanaoona wawezw kuelezea mapicha kwa wenzao wasioona. Wote kwa pamoja watanufaika. Tunaweza kusaidia kwa kuhakikisha kuwa vitabu vya 'Braille' vina kursa za ki-braille na kurasa za kawaida kwa kila karatasi ya kitabu. Kwa njia hii wanaoona na wasioona watajua kuwa wanasoma kwenye ukurasa mmoja.

Kitu kingine cha kufanya ni kutengeneza kaseti ya kusikiliza ambayo inakuwa na sauti zinazoshabihiana na picha. Mathelani, kama kitabu kina picha ya simba, kaseti ya sauti inakuwa na sauti ya simba ya kuunguruma, na mtoto asiyeona anaweza kusikiliza sauti tu wakati yule anaueona anakuwa anatafiti na kuelezea picha. Hata hivyo watoto wanaoona, huelewa vizuri zaidi wanaposikiliza kaseti hizo. Na kwa kweli hatuwezi kugharimia 'Braille' au kaseti, tunapaswa kuwapa mafunzo walimu kuhusu namna ya kufundisha watoto wanaoona na wale wasioona kuhusu jinsi ya kufanya mazoezi pamoja yatokanayo ha vitabu vya maneno na vile vya mapicha.

Bwana Kalumuna anaratibu Elimu Maalum kwa watu wasioona katika Wizara ya Elimu na Mafunzo Sanifu, Kitengo cha Elimu Maalum, Ni mwenye kiti wa Kituo cha Habari kuhusu Ulemavu na 'Tanzania Braille Audio Trust', na ni mhariri kiongezi msaidizi wa Chama cha Waandishi Tanzania.
Mawasiliano: P.O.Box 77700, Dar es Salaam, Tanzania. Barua-pepe: zefakalu@yahoo.co.uk

Shirika la EENET limedhamiria kuboresha matumizi ya sura/taswira/picha katika Utafiti kwa Vitendo kuhusu Elimu-jumuishi. Ilipendekezwa kuwa njia hiyo haiwatengi kabisa wasioona, na hivyo tumekuwa tukiifanyia uchunguzi zaidi. Masaili haya yametufumbua macho na kuibua mawazo na fikra, na tunahamasisha majadiliano zaidi kuhusu suala hili.

Barua/Barua-pepe zako

Kuacha Shule Kwa Wasichana

Nilihitimu mafunzo ya Ualimu mwaka 2004. Shule yangu ya kwanza, nilibaini kuwa idadi ya wasichana katika darasa la 4 ilikuwa ya kuvutia, lakini nilipopewa darasa la 7 nilishuhudia kupungua kwa idadi yao – karibu kwa nusu. Mwelekeo wa jamii (wajadi) unaopendelea wavulana katika elimu unapingana na sera ya jinsia katika elimu nchini Zambia. Hivyo niliona muhimu sana kubainisha sababu za mzizi wa wasichana kuacha shule. Nilichunguza hali hii kwa kusoma matini mbalimbali na kuongea na watu wa sehemu yangu, na kubaini sababu zifautazo:
Sababu za kifedha; kiwango kidogo cha elimu ya wazazi; hali ya kutujiamini kwa wasichana; mimba katika umri mdogo; mwelekeo mbaya wa walimu kuhusu wasichanana hususan katika masomo ya Sanyas. Nilijitahidi kuwahamasisha wazazi kupeleka watoto wao wa kike shule na kwamba kufanya hivyo kunaweza kuleta maendeleo ya nchi. Baadhi ya wazazi wamebadili mtazamo wao na kutaka wasichana waendelee na masomo. Ningependa kuwasiliana na walimu wengine kuhusu suala hili duniani kote.

Augustine Chulube, Kashitu Middle Basic School, P.O. Box 490025, Kaputa, Zambia.

Toleo lililotolewa katika Muda Muafaka

Asante kwa Toleo la 9 ambalo lilijumuisha makala kuhusu matumizi ya sanaa, dansi na sura au taswira katika Elimu-jumuishi. Ulikuja na habari hizi katika muda maufaka. Mimi ni muigizaji wa tamthiliya ninayefanya kazi na chama cha Uigizaji cha Watoto na vijana Swaziland. Tunatumia maigizo kama stadi ya maisha na kama chombo cha kuelimishia na kufahamisha watu hatari na masuala ya kijamii na ya taifa. Maigizo ya meonekana kuwa chombo chenye nguvu cha kutolea taarifa na kuelimisha jamii. Tuna michezo ya kuigiz kuhusu VVU/UKIMWI tukijumuisha na walemavu. Ninaamini kabisa Maigizo yanaweza kuwa thabiti katika kuwezesha Mtandao wa Elimu. Tungependa kutandawaa katika nchi zote na mashirika yote yanayojihusisha na kazi hii ya Elimu.

Zodwa T. Gama, P.O. Box 472, Mbabane, Swaziland.
Barua-pepe: andrewmoyo2000@yahoo.com

Kutumia Michoro Katika Maisha halisi

Nilikuwa natumia mara nyingi michoro kutoka kitabu cha *"Inclusive Education: Where there are f ew resources"* [Elimu-jumuishi: katika sehemu zenye vifaa vichache]. Dada yangu alinichorea tena picha za vibao kwa ajili ya kutumia wakati wa semina kuelezea tofauti kati Elimu Maalum, Elimu –Unganishi na Elimu-jumuishi. Michoro hiyo ilinisaidia sana. Inawakilisha hali halisi ya maisha ambapo maelezo yangu yalisadifu kwa watu wa viwango vyote vya elimu. Nilimwomba fundi seremala anitengenezee Vibao Vizuri vya kutumia wakati wa kutoa mafunzo. Vibao hivyo vilifanya ile michoro ya kitabuni ilete hisia halisi katika maisha ha kuwasaidia washiriki wasioona kufurahia zaidi. Ifuatayo ni michoro kwa ajili ya wengine kutumia.

Karen Chesterton, kwa sasa anafanya kazi kama Mshauri wa Elimu na Ulemavu katika Wizara ya Elimu nchini Afghanistan, kupitia shirika la UNDP.

Barua-pepe: krchesterton-education@yahoo.com au wasiliana naye kupitia anwani ya posta ya EENET.

Tofauti baina ya elimu maalum, elimu-unganishi, na elimu-jumuishi



Elimu Maalum
Mfumo we elimu kwa Wanafunzi wa 'kawaida' (vibao vya duara) na Mfumo tofauti wa watoto Wenye mahitaji maalum (vibao vya mraba).



Elimu-Unganishi
kujaribu kubadili watoto ili waingie katika mfumo wa kawaida (kuchonga vibao-mraba vienee katika matundu ya vibao-duara.



Elimu-jumuishi
Watoto wote ni tofauti – tunabadilisha mfumo ili wote waingie.



Vibao vya mbao vilivyotengenezwa nchini Afghanistan

Mhariri: nakala za kitabu cha "Inclusive Education : Where there are few resources" (kilichochapishwa na Atlas Alliance) zinapatikana bure kutoka EENET)

Machapisho Muhimu

Capacity Building of Teacher Training Institutions in Sub-Saharan Africa
UNESCO (2005)
(*Kuongeza uwezo wa asasi za mafunzo ya walimu katika ukunda wa Africa kusini mwa jangwa la Sahara*). Ni mafupisho au muhtasari wa tathmini ya asasi za mafunzo ya ualimu na kazi ifanywayo na UNESCO katika kanda hii. Yanapatikana katika Kiingereza/Kifaransa kwenye: http://unesdoc.unesco.org

Developing Inclusive Teacher Education
Tony Booth, Karl Nes e Marit Stromstad (2003)
(kuanzisha Ualimu-jumuishi)
Kitabu hiki kinatoa uchambuzi wa ndani wa jinsi 'elimu-jumuishi' inavyoweza kuingizwa na kuboreshwa katika ualimu, kwa kutumia mifano ya England, Scotland, Norway, New Zealand na Marekani, kimechapishwa na Routledge. Kinapatikana kutoka: Taylor & Franci s Group Ltd; Z.Park Square, Milaton Park, Abingdon, OX14 4RN, UK.
Faksi: +44 (0) 2070176699
Tovuti: www.tandf.co.uk/books
ISBN 0-415303184
Bei: £24.99

Guidelines for Inclusion: Ensuring Access to Education for All
UNESCO (2005)
(Miongozo ya Ujumuishi: Kuhakikisha Elimu ni Kwa Wote)
Chapisho hili linalenga kubadili fikira juu ya ujumuishi, ili kwamba Elimu kwa Wote iwe ni harisi kimatendo. Chapisho hili linasimama kama nyenzo ya sera ya kuunda na kupitia mipango ya Elimu kwa Wote na linaweza kutumika kama msingi wa majadiliano baina ya wapanga sera, wanataaluma/waelimishaji, Mashirika yasiyo ya serikali (NGO,S) na mashirika ya kimataifa yanayopenda kuboresha elimu.
Chapisho hili linapatikana kutoka:
UNESCO
7, place de Fontenoy,
75352 PARIS 07 SP
Tovuti: www.unesco.org/education/inclusive

Guidelines and Recommendations for Reorienting Teacher Education to Address Sustainability
UNESCO (2005)
(Miongozo na Mapendekezo kuhusu Ualimu katika kuthibiti Uendelevu)
Matini hii inaliangalia suala la elimu katika hali endelevu. Mahsusi, inabainisha jinsi programu za ualimu zinavyopaswa kupitiwa upya ili kufiti katika hali na malengo ya kimazingira , kijamii, na kiuchumi.
Matini hii inapatikana kwenye tovuti:
http://unesdoc.unesco.org

id21.org
tovuti hii inajumuisha utafiti wa maendeleo ya kimataifa kwa wapanga sera na wataalam, na ina makala nyingi kuhusu masuala ya elimu ya ualimu.

Inclusive Classrooms: The use of images in active learning and action research
EENET (2005)
(Daraisa-jumuishi: Matumizi ya taswira/picha katika kijifunza kwa vitendo na Utafiti wa Vitendo)
Hii ni ripoti inayotoa maelezo zaidi mradi wa EENET wautafiti kwa vitendo kwa kwa kutumia au kuzingatia picha, ulioshirikisha wanafunzi na walimu wa Mpika nchini Zambia. Inapatikana kutoka EENET.

Inclusive Education E-newsletter
(Toleo la Elimu-Jumuishi kwenye mtandao)
Katika mwezi Mei 2005 shirika la kimataifa la "Healthlink Worldwide and Disability Action Council" Kambodia liliendesha majadiliano ya duara kwa muda wa siku 3 nchini Kambodia. Majadiliano yalihudhariwa na karibu watu 60 waliopendelea elimu-jumuishi. Uzoefu wa na shauka zao vilifanikisha kuanzishwa kwa toleo kwenye mtandao (electronically). Toleo la kwenye mtandao linajumuisha masuala kama: ujumuishi wa watoto wasiosikia katika shule za kawaida, umuhimu wa kuwapa wazazi sauti au mafasi katika shule, walimu walemavu kutumika kama mifano, na fursa za utafiti katika Elimu-jumuishi.
Lilitolewa na Healthlink Worldwide na Susie Miles wa kutoka EENET, kama sehemu ya programu ya utafiti na maarifa kuhusu masuala ya Ulemavu.
Linapatikana kutoka:
www.disabilitykar.net/ie_news/ed_intro.html

Learning from Difference
Mwongozo wa EENET kwa wataalam wanaotaka kutumia utafiti wa vitendo katika kazi zao za elimu-jumuishi sasa unapatikana katika printi (na pia katik CD-ROM) kwa Kiarabu, Kiingereza Kifaransa, Kireno, na Kihispaniola. Vyote vinapatikana EENET.

Teacher Training Initiative for Sub-Saharan Africa (TTISSA)
Mafunzo ya Ualimu barani Afrika kusini mwa jangwa la Sahara]. Shirika la UNESCO lilizindua kipao-mbele kuhusu jitihada (mwaka 2006-2015) kuzisaidia nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara kuunda upya sera za taifa kuhusu mwalimu na ualimu. Ina lengo la kuongeza idadi ya walimu na kuboresha ufundishaji. Nchi 17 zinashiriki katika mkakati huu.
Habari zaidi zinapatikana:
www.unesco.org/education/TTISSA

What Makes Teachers Tick?
VSO (2002)
Ripoti hii ilitolewa kama sehemu ya projekti ya kutangaza VSO-Valuing Teacher's (kuthamini walimu) – Ripoti hii inachauguaza mtizamo wa walimu kuhusu mambo yaneyoathiri motisho wao, na kubainisha sera na mabadiliko ya utekelezaji yanayohitajika kuwatia moisho.
Inepatikana kutoka:
www.vso.org.uk/resources/position_papers.asp

Machapisho mengi muhimu yaliyoorodheshwa humu yanapatikana kwenye mtandao. Wasomaji wa EENET ambao si rahisi kwao kupata mtandao (internet) wanashauriwa kuwasiliana nasi, ili tukutolee nakala, au kukunakilia kwenye CD kutoka kwenye mtandao/kompyuta.

EENET

c/o Educational Support and Inclusion
School of Education
The University of Manchester
Oxford Road
Manchester, M139PL,UK

Tel:+44(0)1612753711
Fax:+44 (0) 161 2753548
Email:info@eenet.org.uk
Web: www.eenet.org.uk